Jumatatu Novemba 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581493

nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com



**ANCELOTTI AMTOA BELLINGHAM ENGLAND** UKURASA 22

UKURASA WA 4

**Makonda:** Mnyeti, Kitwanga malizeni ugomvi msivuruge...



UKURASA WA 19

**Israel** yaeleza sababu mashambulizi hospitali Al Shifa...



# NI MAJANGA

• **Mvua** yaleta athari nyumba, mali, miundombinu yakatika...*Endelea Ukurasa 2*



## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**BITEKO AZINDUA KITUO CHA KISASA CHA KUJAZA GESI ASILIA**



NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amezindua kituo cha kwanza...

**TGNP yataka ongezeko wanawake viongozi madarakani**

UKURASA 4




Sehemu ya nyumba kando ya Barabara ya Bagamoyo zilizokumbwa na mafuriko eneo la Boko Basihaya Wilaya ya Kinondoni Dar es Salaam ambayo yamesababisha biashara kusimama na magari kupita kwa shida kufuatia mvua kubwa iliyonyesha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NECTA yatoa namba udanganyifu mitihani IV UK. 2

**MICHEZO** **GAMONDI ATAJA ILIPO JEURI YAKE YANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Ni majanga mvua yaleta athari

**Salome Kitomari na Elizabeth Zaya**

MVUA kubwa iliyonyesha jana katika Jiji la Dar es Salaam imesababisha athari kwa baadhi ya wakazi wa jiji hilo, huku barabara ya Morogoro eneo la Jangwani ikifungwa kwa muda kutokana na maji yenye taka kujaa barabarani na kusababisha watumiaji kushindwa kupita huku nyumba 21 zikibomoka.

Wananchi wanaoishi kando ya Mto Msimbazi eneo la Tabata na Vingunguti, wamejikuta katika wakati mgumu baada ya sehemu ya nyumba zao kubomolewa na maji hayo ya mvua.

Wakazi wengi wa eneo hilo wamelazimika kukimbia makazi yao kwa kuhofia nyumba wanazoishi kutitia.

"Ninavyoongea na wewe nimeondoka kwenye nyumba yangu, maji yamechukua choo na nusu ya nyumba yangu imeenda na maji, nimebakiwa na vyumba vitatu, hali ni mbaya sana. Tumeelezwa na uongozi wa Serikali ya Mtaa Mfaume kuwa Mkuu wa mkoa atakuja kututembelea," alisema Sophia Rashidi, maarufu kwa jina la Mama Ally anayelea mtoto wake mwenye ulemavu.

"Hapa nimemuondoa mwanangu nimekuja huku Mbagala kwa muumini mwezangu ambaye tunasali wote, ndugu zangu walishanikimbia miaka mingi kutokana ulemavu wa mwanangu," alisema.

"Natamani serikali ingeniona mimi mama ninayeishi huku mabondeni inisaidie nipate eneo jingine nipate hata chumba kimoja niishi na mwanangu huyu ambaye ananitegemea kwa kila kitu," alisema.

Akizungumza na mwandishi wetu, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alisema nyumba 21 zimebomolewa na maji katika eneo la Tabata Liwiti, ambazo ziko kando ya Mto Msimbazi.

"Athari za mvua ni kubwa katika baadhi ya maeneo nyumba, uzio na mageti yamebomoka kutokana na maji, huku miundombinu ya mitaa mbalimbali ikishindwa kupitika," alisema na kuongeza:

"Maeneo ya Liwiti mitaa ya Mfaume nyumba 21 zimeathirika na Mto Msimbazi, Jangwani kulijaa maji watu wakashindwa kupita, huko Kivule, Kipawa baadhi ya nyumba pia zimebomolewa na maji, miundombinu ya barabara imeharibika," alisema.

Aidha, alisema hadi sasa wilaya hiyo haijapokea taarifa zozote za madhara kwa binadamu, huku akiwataka waliojenga kando ya Mto Msimbazi kuhama maeneo hayo kwa kuwa ni hatarishi.

"Nimetembelea maeneo mengi ya wilaya yangu na kuhamasisha hatua za dharura, kushawishi waliojenga pembezoni mwa Mto Msimbazi waondoke kwa sababu mto huo kuta zake ni mchanga, hivyo maji yanaathiri kwa urahisi zaidi.

Kwenye mto maji yamepita mengi kuliko kawaida," alisema Mpogolo.

"Athari nyingine ni baadhi ya vivuko kuharibiwa na kutopitika kabisa, na kwamba maeneo la Kivule, Magole na Ukonga barabara nyingi ambazo ni za kiwango cha changarawe hazipitiki kutokana na mashimo makubwa yaliyojaa maji," alisema.

Maeneo mengine yaliyoathirika ni Boko ikiwamo Nyaishozi, Dawasa, Msikitini, Kalifonia, kwa Mpemba pamoja na maeneo ya Mbweni Teta na Mbweni kijijini.

Mwandishi wa habari hizi alishuhudia nyumba nyingi katika maeneo hayo pamoja na fremu za biashara zikiwa zimejaa maji na kuharibu vitu vilivyokuwa ndani.

Aidha, wafanyabaishara wengi walilazimika kufunga biashara zao baada ya maeneo yao kuelea maji.

Katika eneo la Boko kwa Mpemba maji yalijaa na kupita juu ya barabara na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wenye vyombo vya moto ambao walilazimika kukaa kwa saa kadhaa.

Katika eneo hilo la Boko Msikitini Nipashe lilishuhudia samani za ndani zikiielea kwenye maji huku wakazi wanaoishi katika eneo hilo wakishindwa kutoka ndani baada ya nyumba zao kuzingirwa na maji.

Baadhi ya wakazi wa Boko Kalifonia walisema tatizo kubwa linalochangia maji kujaa katika eneo hilo ni kukosekana kwa mitaro ya kupitisha maji.

"Shida ya barabara hii hakuna mitaro ya maji kwa hiyo maji haya yanatuwama tu hakuna kwa kwenda la sivyo miundombinu ingekuwa vizuri tusingeshuhudia haya mafuriko tunayoyaona sasa," alisema Hezron Eliudi.

"Kama unavyoona nyumba zimezingirwa maji na mule ndani kuna watu. Tunachoomba hizi mvua zisiendelee zaidi ya pale maana hali itakuwa mbaya zaidi.

Akizungumzia utatuzi wa kudumu, Mkuu huyo wa Wilaya, alisema serikali imeshapata fedha za mradi wa DMDP awamu ya pili ambao utajenga barabara za mitaa kwa kiwango cha lami.

"Kwa eneo la Jangwani tayari kuna mradi wa daraja ambao utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 600, ambao utaboresha mfumo wa maji yapite kwa urahisi kwenda baharini.

Tumeshakamilisha tathimini na watu watalipwa fidia kupisha upanuzi wa Mto Msimbazi. Wataalam wametuambia mto huo eneo la Jangwani ukijengwa maji yakijaa hayawezi kusababisha madhara kwa sababu daraja litakuwa na kina kirefu na kingo imara, hili litakuwa suluhisho la muda mrefu."

Aidha, alisema hatua nyingine ni kuendelea kuimarisha kamati za mitaa, kata ili kusaidia watu wanapopata tatizo na kwamba kwa siku ya jana wamefanyakazi bila kuchoka na kutambua waliopata maafa.

Nipashe ilimtafuta Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, kupata tathmini ya jiji kwa ujumla, lakini simu yake iliita mara tatu bila kupokelewa.



Mafuriko yaliyotokana na mvua zinazoendelea mkoani Dar es Salaam. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

MTIHANI KIDATO CHA IV

# NECTA yataja namba maalum kuripoti udanganyifu

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA), limetangaza namba maalum ya kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya udanganyifu wakati wa mtihani wa Kidato cha Nne, 2023 pamoja na wa maarifa, unaotarajiwa kuanza leo nchini ukihusisha jumla ya watahiniwa 572,338.

Akitangaza jana kuanza kwa mtihani huo, Katibu Mtendaji wa Baraza, Dk. Said Mohamed, aliwataka wadau wa elimu wakiwamo wazazi watakapoona vitendo vya udanganyifu vikifanyika, wapige simu namba 0759360000 au watume ujumbe kwa barua pepe esnecta@necta.go.tz kwa hatua zaidi.

Alisema mtihani huo unatarajiwa kuanza leo hadi Novemba 30 katika jumla ya shule za sekondari 5,371 na vituo vya watahiniwa wa kujitegemea 1,798.

Dk. Mohamed alisema watahiniwa 572,338 wamesajiliwa kufanya na kati yao, watahiniwa wa shule ni 543,386 na wa kujitegemea ni 28,952.

"Kati ya watahiniwa wa shule 543,386 waliosajiliwa mwaka 2023, wavulana ni 250,237 sawa na asilimia 46.05 na wasichana ni 293,149 sawa na asilimia 53.95. Watahiniwa wa shule wenye mahitaji maalum ni 614 na kati yao 283 ni wenye uoni hafifu, 24 ni wasioona, 135 wenye ulemavu wa kusikia, 11 ni wenye ulemavu wa akili na 161 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwili," alisema.

Alisema mwaka 2022, jumla ya watahiniwa wa shule waliosajiliwa walikuwa 534,753, na kufanya ongezeko la jumla ya watahiniwa 8,633 sawa na asilimia 1.61 kwa mwaka huu ikilinganishwa na mwaka jana.

Kwa mujibu wa Dk. Mohamed, kati ya watahiniwa wa kujitegemea 28,952 waliosajiliwa, wavulana ni 11,867 sawa na asilimia 40.99 na wasichana ni 17,085 sawa na asilimia 59.01.

Alisema watahiniwa wa kujitegemea wenye mahitaji maalum wako wanane, wenye uoni hafifu ni wanne na wasioona wapo wanne.

Pia, alisema jumla ya watahiniwa 10,927 wamesajiliwa kufanya Mtihani wa Maarifa (QT) 2023, wanaume ni 4,020 sawa na asilimia 36.79 na wanawake ni 6,907 sawa na asilimia 63.21.

"Watahiniwa wa maarifa wenye mahitaji maalum ni 38 ambapo wote ni wenye uoni hafifu. Mwaka 2022 jumla ya watahiniwa waliosajiliwa walikuwa 12,110, hivyo kuna upungufu wa jumla ya watahiniwa 1,183 sawa na asilimia 9.77 kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na mwaka 2022," alisema.

Alisema Baraza halitarajii kuona mtahiniwa yeyote akijihusisha na vitendo vya udanganyifu na atakayebainika matokeo yake yatafutwa kwa mujibu wa kanuni za mitihani.

Pia, alisema Baraza litakifuta kituo chochote cha mtihani endapo litajiridhisha pasipo shaka uwapo wake kuhatarisha usalama wa mtihani. "Wakuu wa shule wahakikishe wanatekeleza majukumu yao ya usimamizi kwa kuzingatia mwongozo wa usimamizi uliotolewa na Baraza la Mitihani na kuepuka kuingilia usimamizi wa watahiniwa ndani ya vyumba vya mitihani," alisema.

Dk. Mohamed alisema Baraza limewaomba wananchi kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote asiyehusika na mtihani kuingia kwenye maeneo ya shule katika kipindi chote cha mtihani.

Aliwataka watoe ushirikiano katika kudhibiti vitendo vyovyote vya udanganyifu katika mtihani wa Maarifa na Kidato cha Nne mwaka 2023.

"Baraza halitasita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayebainika kujihusisha na kusababisha udanganyifu kufanyika kwa mujibu wa sheria za nchi yetu," alisema.

Alisema pamoja na maandalizi yote muhimu yaliyofanyika, Kamati za Mitihani za Mikoa na Halmashauri zihakikishe kuwa usalama wa vituo vya mitihani unaimarishwa na vinatumika kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa na Baraza.

Pia amewataka wasimamizi wote waliopangwa kusimamia uendeshaji wa mtihani katika kituo husika wanafika kwa wakati katika vituo husika.

**HABARI KITAIFA**

# Anayedaiwa kumnyonga mpenzi aonyesha polisi alimpomfukia

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita imeanza kusikiliza kesi ya mauaji inayomkabili mkazi wa Lunzewe, Petro Kinasa (30), ambaye ameshtakiwa kwa kosa la kumuua Esta John kwa kumnyonga shingo kisha kuchimba shimo na kumfukia.

Mshtakiwa alipandishwa kizimbani mbele ya Jaji wa Mahakama hiyo, Liliani Itemba.

Aliposomewa shtaka lake, alikana kuhusika na kuwekwa mahabusu katika Gereza la Geita.

Upande wa Jamhuri ulikuwa ukiongozwa na mawakili watatu wa serikali ambao ni Godfrey Odupoy, Mussa Mlawa na Verena Mathias, wote kwa pamoja walidai kuwa na mashahidi wanne na wako tayari kwa kuwasikiliza.

Jaji Itemba alikubaliana na ombi hilo na kuliza upande wa utetezi ukiongozwa na wakili wa kujitegemea, Erick Lutehanga, kama yuko tayari kwa kusikiliza mashahidi wanne wa upande wa Jamhuri. Alijibu kuwa yuko tayari kusikiliza ushahidi.

Shahidi wa kwanza wa upande wa Jamhuri, SGT Adriano (54) akiongozwa na Wakili wa Serikali, Godfrey Odupoy, alidai Juni 23, 2021 alikuwa kazini kwake katika kituo cha polisi Lunzewe majira ya saa tisa usiku na kuletwa mshtakiwa kwa kosa la mauaji ya kumuua mpenzi wake kwa kumnyonga shingoni kwa kutumia kamba ya katani.

Adriano alidai ilipofika majira ya saa 11 alfajiri alipewa maagizo na mkuu wa kituo hicho kwamba amuandikie mshtakiwa maelezo.

Mshtakiwa huyo alimueleza polisi Adriano kuwa marehemu Esta John alikuwa mpenzi wake na aliwahi kumpatia Sh. 70,000 kwa ajili ya biashara.

Alidai Juni 15, 2021 majira ya saa tatu asubuhi mshtakiwa alifika nyumbani kwa mpenzi wake na kuomba aende kumsaidia kuvuna mpunga na wakaondoka wakiwa watu watatu; mshtakiwa, Esta na mtoto ambaye alimtaja kwa jina moja la Winfrida.

Alidai walipofika porini mshtakiwa alichukua kamba ya katani na kumnyonga shingoni mpenzi wake na kufariki dunia papo hapo. Baada ya kumuua aliende kwenye majaruba ya mpunga na kuchukua jembe kisha kuchimba shimo la futi tatu na kumfukia.

Alidai pia alichukua kanga ya marehemu na kumziba mtoto mdomo na pua na kufariki dunia papo hapo kisha kumtupa kichakani.

Aliendelea kudai baada ya kumueleza tukio zima la mauaji hayo, alimuuliza anakumbuka alipomzika mpenzi wake na mtoto wake? Mshtakiwa alijibu ndiyo na shahidi Adriano aliacha kuandika maelezo ili aende kumuonyesha alipomfukia marehemu na alipomtupa mtoto wa marehemu.

“Mimi pamoja na askari polisi wenzangu tuliongozana na mshtakiwa hadi kwenye pori alipomfukia marehemu Esta John, tulipofika mshtakiwa alituonyesha na tulipofukua kweli tulikuta mwili wa marehemu ukiwa na kamba ya katani shingoni, tuliuchukua na kuupeleka katika chumba cha kuhifadhia maiti katika kituo cha afya Unyovu kilichopo Wilaya ya Bukombe Mkoa wa Geita,” alidai.

Pia, mshtakiwa aliwaonyesha askari polisi sehemu alipokuwa ametupa mwili wa mtoto wa marehemu Esta na kukuta mifupa na fuvu la kichwa.

Shahidi alidai, baada ya mshtakiwa kuwaonyesha sehemu hiyo alirudi na mshtakiwa hadi kituo cha polisi na kuendelea kuandika maelezo ya mshtakiwa na alipomaliza alimpeleka mahabusu.

Jaji Itemba alimuuliza Wakili wa Kujitegemea Erick Lutehanga ambaye anamtetea mshtakiwa kama ana maswali ya kumuuliza shahidi wa upande wa Jamhuri, Wakili huyo alijibu kuwa ana maswali kama ifuatavyo;

**Wakili:** Wakati unatoa ushahidi wako ulisema mshtakiwa aliwaua watu wawili?

**Shahidi:** Ndiyo aliwaua watu wawili.



Mshtakiwa Petro Kinasa (30), akiwa chini ya ulinzi mkali wa polisi. **PICHA: JACTON NGELLY**

**Wakili:** Hilo kaburi lilikuwa na futi ngapi?

**Shahidi:** Kaburi lilikuwa na futi tatu.

**Wakili:** Shahidi wakati unatoa ushahidi wako haujaeleza mshtakiwa alitumia muda gani kuchimba kaburi na kufukia?

**Shahidi:** Ndiyo sijaeleza.

Wakili: Muda gani alipomuua na kufukia na nyinyi mlienda kufukua lini?

**Shahidi:** mshtakiwa alimuua na kufukia Juni 15 mwaka 2021 na sisi tulienda kufukua Juni 23 mwaka 2021.

**Wakili:** Wakati ukitoa ushahidi wako haujaeleza hali ya mshtakiwa

**Shahidi:** Ndiyo sijaeleza hali ya mshtakiwa.

**Wakili:** Wakati unatoa ushahidi wako haukutoa kitabu cha majina ya washtakiwa waliokuwepo hapo kituoni.

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Wakati ukitoa ushahidi wako haukutuambia ulikuwa na wakina nani ambao uliongozana nao eneo la tukio

**Shahidi:** Ndiyo sikueleza.

Baada ya Wakili Lutehanga kumaliza kumuuliza shahidi wa upande wa Jamhuri, Jaji Itemba alimuuliza Wakili wa Kujitegemea ana maswali ya kusawazisha, Wakili wa serikali Verena Mathias, alijibu kuwa anayo maswali kama ifuatavyo;

**Wakili:** Maelezo unayoyatoa hapa mahakamani uliyatoa wapi?

**Shahidi**: Maelezo ninayoyatoa hapa mahakamani niliambiwa na mshtakiwa.

**Wakili:** Mbele ya mahakama hii ushahidi wako unahusiana na nani?

**Shahidi:** Ushahidi wangu unahusiana na maelezo ya onyo ya mshtakiwa.

Baada ya Wakili wa Serikali Mathias kumaliza kumuuliza shahidi wake maswali alidai hapo mahakamani kuwa kuna shahidi mwingine ambaye ni daktari aliyefanya uchunguzi wa mwili wa marehemu Esta, Jaji Itemba alimueleza Karani wa Mahakama hiyo amuite shahidi wa tatu wa upande wa Jamhuri.

Shahidi wa pili wa upande wa Jamhuri Mathayo Marelemba (39) ambaye ni daktari wa kituo cha afya Unyovu, Wilaya ya Bukombe, akiongozwa na Wakili wa Serikali Verena Mathias, alidai Juni 23, 2021 alipigiwa simu na Mganga Mfawidhi wa kituo hicho cha afya kwamba aongozane na maaskari polisi kwenda kwenye tukio la kufukua mwili.

Marelemba alisema walipofika eneo la tukio walifukua mwili wa marehemu Esta ukiwa na kamba ya katani shingoni na ukiwa na harufu mbaya na kuupeleka Kituo cha Afya Unyovu na alipoufanyia uchunguzi ilibainika kuwa marehemu Esta hakuwa na nguo za ndani pia alinyongwa na kamba ya katani shingoni na kukosa hewa na kufariki dunia.

Shahidi huyo alidai Juni 24, 2021 alijaza fomu ya uchunguzi wa mwili wa marehemu Esta kisha kumkabidhi Mkuu wa Kituo cha Polisi Lunzewe.

Baada ya shahidi wa pili wa upande wa Jamhuri kumaliza kutoa ushahidi wake, Jaji Itemba alimuuliza Wakili wa Kujitegemea, Lutehanga ana maswali ya kumuuliza shahidi wa upande wa Jamhuri, Wakili huyo alijibu kuwa anayo.

**Wakili:** Mwili wa marehemu ulikuwa umeharibika?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Kilichokuonyesha kwamba marehemu alinyongwa ni kamba ya katani shingoni?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Mbona hati ya uchunguzi wa mwili wa marehemu Esta John haina muhuri?

**Shahidi:** Muhuri upo lakini nilisahau kuweka.

Wakili wa Serikali Mathias aliomba mahakama hiyo ipange tarehe nyingine ili waweze kuendelea na mashahidi wengine waliobaki.

Jaji Itemba alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Novemba 13 (leo) kwa ajili ya kuendelea kusikiliza mashahidi wa upande wa Jamhuri.

Akisoma hati ya mashtaka Karani wa Mahakama hiyo, Gladness Mnjari, alidai tarehe isiyojulikana mwezi Juni mwaka 2021 katika Kijiji cha Kanembwa, Wilaya ya Bukombe mshtakiwa anadaiwa kumuua Esta John kwa kumnyonga shingoni na kamba ya katani na kufariki dunia papo hapo.


**KUPOTEA KWA CHETI**



**LIGHT KITURURU CHEDIEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4140/0040** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SIMBOMU SEKONDARI mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/34354/2023.**

**KUPOTEA KWA CHETI**



**JULIETH JAPHET RUTAIHWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4967/0040** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. ALOYSIUS GIRLS' SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/34409/2023**.



FOMU MIRATHI - 2

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 1703/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ALLY GALAFUNGA MGIMWA WA KEKO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MOHAMED KHAMISI MAGALI**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 mwezi 11 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetokewa leo tarehe 10 mwezi 11 mwaka 2023.

HAKIMU



**ABBOTT FUND TANZANIA**
**(NGO Certificate of Registration Number 00483)**

**PUBLIC NOTICE MADE PURSUANT TO REGULATION 13 (A) OF THE NON-GOVERNMENTAL ORGANISATION ACT (AMENDMENTS) REGULATIONS 2018 MADE UNDER GOVERNMENT NOTICE NO. 609 OF 19TH OCTOBER 2018**

**WHEREAS** Regulation 13 (a) of the abovementioned regulations requires that all non-governmental organisations in Tanzania publish biannually funds received and their expenditure in a widely circulated newspaper which are accessible by the targeted beneficiaries as part of financial transparency and accountability compliance requirements.

**IN VIEW OF THE ABOVE,** we wish to make the following public disclosure of the funds approved for 2023 activities and their proposed expenditure, which publication covers the reporting period from 1st July 2023 to 31st December 2023:

| Project Area Expenditure | Amount in (USD) |
|---|---|
| **Muhimbili National Hospital Sustainability Strategy Support:** Includes support to Leadership Capacity-Building. | 150,000 |
| **Emergency Medicine Regional and District Amplification:** Includes support to MNH Emergency Medicine and EMD infrastructure project. | 600,000 |
| **Village Emergency Care Model** in Dodoma, Mbeya and Tanga. | 375,000 |
| **Building Livelihoods**: Includes support to National Children's Centre in Dodoma. | 270,000 |
| **Mapatano Project:** Includes infrastructure project at Mapatano Secondary School. | 2,400,000 |
| **Administration:** Includes travel, office costs and program implementation staff. | 1,991,000 |
| **Total Funds received from Abbott Fund, Chicago IL, USA for the year 2023.** | **5,786,000** |

**ISSUED BY**
**EXECUTIVE DIRECTOR**
**ABBOTT FUND TANZANIA**

217707902

# TGNP yataka ongezeko wanawake madarakani

**Na Salome Kitomari**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), umezindua Ilani ya Madai ya Wanawake katika uchaguzi ijulikanayo kama Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake - Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025.

Lengo la ilani hiyo ni kudai mabadiliko ya mifumo kandamizi inayohalalisha ubaguzi wa wanawake katika uchaguzi kama wapigakura na wagombea wa nafasi mbalimbali kuanzia taifa hadi serikali za mitaa.

Uzinduzi huo ulifanyika mwishoni mwa wiki wakati wa kuhitimisha Tamasha la 15 la Jinsia na Miaka 30 ya TGNP la TAPO la Ukombozi wa Wanawake, makao makuu ya mtandao huo Mabibo Jijini Dar es Salaam.

Kauli mbiu ya ilani hiyo ni Ajenda ya Mwanamke, Turufu ya Ushindi.

Siku ya zinduzi huo ndipo Bunge lilipotisha mabadiliko ya sheria mbalimbali za uchaguzi ambazo pamoja na mambo mengine zimeweka msingi wa usawa wa kujinsia kwenye vyama vya siasa ili kutoa ushindani sawa kwenye jukwaa la kisiasa katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, mwanaharakati mkongwe wa haki za wanawake na usawa wa kijinsia, Profesa Ruth Meena, alisema msingi wa ilani hiyo ni kuendeleza harakati za wanawake watetezi wa haki za ushiriki katika uongozi wa kisiasa tangu nchi ilipopata uhuru mwaka 1961 hadi leo.

Profesa Ruth ambaye pia ni mwanachama wa TGNP, alisema ilani hiyo ni ya sita ya madai ya wanawake katika uchaguzi, na kwamba ya kwanza ilikuwa mwaka 2000 ikijulikana kama Ilani ya wapigakura.

Nyingine ni ya mwaka 2005, ya tatu ni ya mwaka 2010, ya nne ni ya mwaka 2015 ya tano ni ya mwaka 2020.

"Maandalizi ya ilani zote sita yaliongozwa na TGNP kwa kupitia Mtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi unaoratibiwa na Mfuko wa Ufadhili wa Wanawake Tanzania (WFT_T) pamoja na Mitandao mingine ya Tapo la Ukombozi wa Wanawake Kimapinduzi," alisema Prof. Ruth.

Kwa mujibu wa mwanaharakati huyo, walengwa wa kwanza wa ilani hiyo ni wanawake ambao ni wapiga kura, wenye nia na haki ya kushiriki katika uchaguzi na hatimaye kushiriki katika kuliongoza taifa kwenye maeneo mbalimbali.

"Tunapaswa kuwa na sauti moja na kuwa na ajenda moja ya kudai mabadiliko ya mfumo kandamizi wenye ubaguzi. Kwa pamoja tunasema hatuwezi kujenga demokrasia thabiti kama uchaguzi wetu sio huru na haki kwa jicho la jinsia," alibainisha.

Aidha, alisema ilani hiyo inaihusu serikali iliyopo madarakani, taasisi na vyombo vyote vinavyohusika na uchaguzi viwajibike kwa kuzingatia matamko ya kimataifa na kikanda, mikataba, itifaki na misingi ya kikatiba iliyoanishwa kwenye Dira ya Taifa 2025.

"Ilani inaitaka serikali kuchukua hatua za makusudi kusawazisha mazingira ya uchaguzi ili wanawake waweze kushiriki bila vikwazo vinavyowabagua," alisema.

Alisema: "Walengwa wengine ni vyama vya siasa ambavyo katika muktadha wa uchaguzi vina uwezo mkubwa wa kuamua ni nani aingie kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi, ni nani afungiwe milango na ni nani aungwe mkono hadi hatua za ushindi."

Akizungumza na waandishi wa habari,Mwenyekiti wa Bodi ya TGNP, Gemma Akilimali, aliishauri serikali kuboresha mfumo na utaratibu wa utoaji mikopo ya halmashauri na mafunzo ya uendeshaji miradi/bishara na utunzaji wa fedha kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ili kupunguza urasimu na kuwezesha upatikanaji rahisi wa taarida kuhusu fursa kwa makundi hayo.

Aidha, alipendekeza wajumbe wa Kamati za Vijiji kuhamasisha na kutumia fursa mbalimbali za kujiongezea uwezo na uelewa kuhusu elimu ya afya ya uzazi, ili kuwa mstari wa mbele kusimamia kwa ufanisi utaoji wa mikopo hiyo.

Akilimali aliitaka serikali kuweka kipaumbele upatikanaji wa vifaa tiba na idadi ya kutosha ya watoa huduma kwenye zahanati na vituo vya afya.

Pia TGNP imeitaka serikali kuchagiza mapitia na marekebisho ya sheria za uchaguzi wa serikali za mitaa na kanuni zake, ili kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake na makundi mengine kujumuishwa na kushiriki kikamilifu kugombea nafasi za uongozi na ngazi za maamuzi.

Ijumaa iliyopita bunge lilipitisha mabadiliko ya sheria ya tatu za uchaguzi ambazo zimekuja na muunda mpya wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kuwa na kamati itakayosaili wajumbe wa tume hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita (kushoto) akimkabidhi pembejeo za kilimo ruzuku, mkulima Bertha Yohana, zilizotolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Kahama iliyofanyika katika kituo cha Mwendakulima kinachofadhiliwa na Barrick mwishoni mwa wiki.Wengine pichani ni watendaji wa kituo hicho na Maofisa kutoka manispaa hiyo. Wakulima wapatao 90 walipatiwa mkopo wa pembejeo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

# Makonda: Mnyeti, Kitwanga malizeni ugomvi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amemtaka Mbunge wa Jimbo la Misungwi, Alexander Mnyeti, kukaa na aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Charles Kitwanga, kukutana na kumaliza ugomvi.

Makonda alitoa agizo hilo wakati akisalimia wananchi wa Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza kuwa hatokubali kuona vurugu ndani ya chama kwa kuwa yeye ni mzaliwa wa eneo hilo na viongozi hao wanatakiwa kuwa mfano kwa wilaya nyingine nchini.

"Hatutokubali mlete mpasuko ndani ya chama sababu ya ugomvi wenu, nakutuma uende kwa Kitwanga mkazungumze na kusameheana, wewe ni zao lake hatutaki mlete matabaka ndani ya CCM," alionya Makonda.

Katika hatua nyingine Makonda alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya kupokea taarifa ya ujenzi wa daraja la JPM lenye urefu wa kilomita tatu na kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 700, kwa kufikia asilimia 80 ya ujenzi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alisema daraja hilo lilitakiwa kukamilika Februari, mwaka 2024, kutokana na changamoto zilizojitokeza linaweza kukamilika Agosti, mwakani.

"Kutokana na adha ya nyumba za wananchi wanaozunguka eneo la ujenzi wa daraja kupata mtikisiko tutakaa na wenzetu wa China ili tuone namna ya kulipa fidia kwa nyumba zilizopasuka," alisema Makalla.

Mbunge wa Jimbo la Sengerema, Hamis Tabasamu, alisema, Rais Samia Hassan, ametoa kibali cha ujenzi wa kivuko kipya cha Buyagu na Mbalika ambacho kitatumiwa na wananchi wa Wilaya ya Misungwi na Sengerema.

"Tunamshukuru Rais ni miaka 40 imepita wananchi wa maeneo hayo hawakuwa na kivuko, kutokana na vivuko vilivyokuwepo kuzama mwaka 1972 ambavyo ni MV Mapaja na MV kitenge vilisababisha tabu kubwa kwa wananchi," alisema Tabasamu.

# CCM yaagiza stendi Mwembeyanga ifunguliwe leo

**Na Beatrice Shayo,** SENGEREMA

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, ameagiza kufunguliwa kwa stendi ya mabasi ya Mwembeyanga iliyopo Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza baada ya kufungwa kwa madai ya rushwa na uzembe.

Aliagiza stendi hiyo ifunguliwe leo wakati wa mkutano wa hadhara na wananchi na kusema kuna tatizo la kutofunguliwa kwa stendi hiyo kutokana na uzembe na rushwa.

Mkurugenzi Shekidele alisema anaomba kutoa ahadi kwamba stendi hiyo itafunguliwa ndani ya wiki hii.

"Ningependa kufahamu kinachokupa sababu ya kufungua wiki hii ni nini? Ni taratibu, kanuni au ni kitu gani? Ili tufanye kwa mujibu wa sheria embu tuambie," alihoji Makonda.

Akijibu Mkurugenzi huyo alisema wiki iliyopita walikutana na Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla na alitoa maelekezo kwamba stendi hiyo ifunguliwe haraka na wao walikuwa na kikao mwishoni mwa wiki.

"Leo ni Jumapili kesho naondoka Mwanza kama Mkuu wa mkoa alishakuja akatoa maelekezo hayo nisikilize mzee," alisema Makonda.

Aidha, alisema kuna hospitali imekamilika inasuburiwa kufunguliwa alimwambia Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla kuwa maelekezo ya chama wiki ijayo hospitali hiyo iwe imefunguliwa ili wananchi waendelee kupatiwa huduma.

Ofisa Ardhi Wilaya ya Sengerema, Seth Lianga, alisema kuna changamoto ya hati ya stendi ya Bukala mpaka sasa hawajalipwa fidia na wiki iliyopita Makalla alielekeza Mkurugenzi kulipa fidia ili wapate uhalali wa kutengeneza hati.

Alisema kwa upande wa soko kuu wameshaandaa rasimu za hati wanasubiri ndani ya wiki mbili zitakuwa zimeshatoka.

"Unasema ukweli ndani ya wiki mbili hati unaenda kuchukua wapi Kamshina wa Ardhi Mwanza haya kesho ukachukue hati hakuna cha wiki mbili kutoka hapa kwenda Mwanza hata kama hauna lifti nutakubeba katika gari yangu," alisema Makonda.

HABARI KITAIFA



Waziri wa Sheria na Katiba, Balozi Dk. Pindi Chana (kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (katikati) Waziri wa Viwanda na Biashara wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Omary Shabaan (kulia) wakijadiliana jambo wakati wa hafla maalum iliyoandaliwa na Benki ya NMB iliyoikutanisha benki hiyo na Taasisi za Sheria Mkoa wa Dar es Salaam, ikiwa ni muendelezo wa ushirikiano baina ya pande hizo mbili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko azindua kituo cha kisasa cha kujaza gesi asilia

**Na Frank Monyo**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amezindua kituo cha kwanza cha kisasa cha kujazia gesi asilia kwenye magari na karakana ya kuweka mfumo wa gesi asilia ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa mipango ya serikali kuchochea matumizi ya gesi asilia kama nishati safi na salama kwa mazingira.

Uzinduzi wa kituo hicho kinachojulikana kama 'Master Gas' umefanyika mwishoni mwa wiki Pugu na kuhudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, Balozi Sherif Ismail wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, Balozi Isaac Njenga wa Jamhuri ya Kenya, Balozi Fred Mwesigye wa Jamhuri ya Uganda, Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya TAQA, Pakin Kafafy.

Mradi huo umeanzishwa na Kampuni ya TAQA Dalbit kupitia ubia kati ya TAQA Arabia na JCG Oil & Gas ikiwa ni jitihada za kuimarisha adhma ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kuongeza matumizi ya akiba yake ya gesi asilia, ambayo inatoa mbadala wa mazingira safi na unafuu kwa watumiaji.

Dk. Biteko akizungumza katika uzinduzi huo alisema, kujengwa kwa kituo hicho na TAQA Arabia na washirika wao JCG Oil & Gas niutekelezaji wa maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa na maono ya kuleta wawekezaji nchini wakiwemo wanaowekeza kwenye Sekta ya Nishati, hivyo ameahidi kuwa Wizara itafanyia maelekezo yake ili kutekeleza maono yake.

Alisema serikali inaweka msukumo mkubwa kwenye matumizi ya gesi ya asilia yakiwamo magari, mitambo ya viwandani, kituo hicho ni kuonesha azma ya serikali ya kuhakikisha kuwa gesi inayopatikana Tanzania inatumika ndani ya nchi kwanza.

Dk. Biteko alisema, kituo hicho kina uwezo wa kujaza gesi kwenye magari 800 kwa siku na kina pampu sita zitakazojaza gesi kwenye magari sita kwa maramoja na ujazaji wa gari moja utakuwa ni wa dakika tatu.

Alisema kampuni hiyo inatarajia kujenga vituo 12 vya CNG jijini Dar es Salaam ili kuwa na vituo vingi zaidi vya kujazia gesi kwenye magari.

Kampuni hiyo kwa kushirikiana na TPDC wapo kwenye majadiliano ili kujenga vituo vidogo vya gesi ya kusindika (LNG) na kutoa jijini Dar es Salaam na kupeleka kwenye mikoa mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAQA Arabia, Pakinam Kafafi, alisema; "Tunayo furaha kutangaza uzinduzi wa kituo cha kujaza gesi asilia cha Tanzania na cha kubadilisha mfumo wa magari Dar es Salaam. Hii ni hatua kubwa kwa TAQA Arabia tunapoungana na JCG pamoja na serikali ya Tanzania, ikiwa ni juhudi muhimu katika dhamira yetu ya kuhudumia mahitaji ya nishati nchini huku tukiendana na dira ya nishati ya taifa," alisema na kuongeza kuwa;

Mkurugenzi Mtendaji wa JCG, Rikin Shah, alibainisha kuwa; "JCG Oil & Gas tumefutiwa na jitihada za TAQA Arabia na Serikali ya Tanzania kutumia rasilimali za taifa za gesi asilia kwa kuanzisha kituo chetu cha kwanza cha TAQA Dalbit. Kupitia ushirikiano wa mradi huu tunaamini kuwa dhamira yetu ya kujenga mustakabali endelevu kwa dira yetu.

"Utoaji wa mchanganyiko wa gesi asilia na nishati iliyopo itatusaidia kusonga mbele zaidi kwa dira yetu.

Tumekuwapo Tanzania kwa miaka 15 sasa tukitoa ufumbuzi wa mafuta kupitia kampuni yetu ya Dalbit Tanzania, iliyoanzishwa mwaka 2008. Gesi asilia ni chanzo cha nishati safi mbadala ikilinganishwa na petroli na dizeli. Ikija wakati ambapo nchi inakabiliwa na kupanda kwa bei ya mafuta na gharama za maisha, bila shaka wamiliki wa vyombo vya moto watafurahi kujua kwamba kituo hiki cha gesi asilia kitatoa mbadala nafuu na kwamba wanaweza kubadilisha mfumo wa magari yao kwa urahisi katika kituo chetu," alisema

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo aliishukuru Wizara ya Nishati kwa kutekeleza maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan ya usambazaji nishati katika maeneo yote ikiwamo gesi asilia.

# Wachimbaji wadogo hatarini kuangukiwa miamba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika mgodi wa Mwakitolyo wapo hatarini kuangukiwa na miamba iliyobainika kuning'inia katika machimbo hayo.

Timu ya wataalamu iliyoundwa na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, ya kufanya uchambuzi wa mikataba na usalama wa wachimbaji wadogo katika machimbo hayo, wilayani Shinyanga, iligundua hatari hiyo.

Akiwasilisha taarifa hiyo juzi kwa Waziri wa Madini, Mwenyekiti wa Timu hiyo, Mhandisi Ally Samaje, alisema wamebaini kwamba eneo hilo la uchimbaji linahitajika kukatwa miamba inayoning'inia na kurekebisha maduara ili wachimbaji wachimbe kwa usalama zaidi.

Alisema kamati hiyo licha ya masuala ya kiusalama, pia imebaini uchimbaji wa pamoja (co-existence) kati ya wachimbaji wadogo na wabia kupitia mwongozo wa uchimbaji utakaosimamiwa na Wizara ya Madini, utasaidia kuongeza kasi ya uzalishaji madini na kuchangia pato la taifa.

Akipokea taarifa hiyo, Waziri Mavunde alimwelekeza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini Msafiri Mbibo, kusimamia kwa ukaribu urekebishaji wa maduara na maeneo yenye miamba inayoning'inia kwa usalama wa wachimbaji wadogo na kuongeza uzalishaji wa madini.

"Usalama katika maeneo ya uchimbaji ni suala muhimu ambalo lazima tulipe uzito mkubwa, naelekeza maeneo yote hapo Mwakitolyo yaliyo chini ya ubia wa msaada wa kiufundi, yarekebishwe dosari zote za kiusalama ili wachimbaji wadogo wafanye shughuli za uchimbaji katika mazingira ambayo ni salama," alisema Mavunde.

Aliwahakikishia wachimbaji hao wakati wa shughuli hizo za marekebisho, hakuna atakayeondolewa katika eneo lake.

Katika hatua nyingine alisema, Rais Samia amewaelekeza kusimamia wachimbaji wadogo pamoja na kuwapatia leseni na maeneo ya uchimbaji, na kuwasaidia upatikanaji wa mikopo ili kuongeza tija katika shughuli zao za uzalishaji madini na kuchangia pato la taifa.

Naibu Kamishina Msaidizi wa Madini kutoka Wizara ya Madini, Terence Ngole, akiwa katika Jukwaa la Uziduaji madini, mafuta na gesi asilia hivi karibuni, jijini Dodoma, alisema wachimbaji wadogo kwa sasa wamekuwa na mchango mkubwa katika kuchangia pato la taifa ikiwa wanachangia asilimia 40.

# Wauawa kwa mkuki wakidaiwa kuiba ng'ombe

**Na Said Hamdani,** LINDI

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Mipoto, Kijiji cha Ngorongoro, Kata ya Namayuni, tarafa ya Kipatimu, wilayani Kilwa mkoani Lindi, Zuberi Mpiri (40) na Shaibu Mwangu (25), wameuawa kwa kuchomwa na mkuki kwa madai ya wizi wa mifugo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka eneo la tukio zilizothibitishwa na viongozi mbalimbali wa serikali, tukio hilo lilitokea Novemba mosi, mwaka huu.

Miili ya watu hao iligunduliwa na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Yomanga, Kijiji na Kata ya Namayuni, Tarafa ya Kipatimu, wilayani humo, Ally Swalehe Mbichi (40), baada ya kuhisi harufu kali.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi, baadhi ya mashuhuda (majina yamehifadhiwa), walisema chanzo cha vifo vyao ni kudaiwa kujihusisha na wizi wa ng'ombe dume aliyechinjwa na nyama yake kuuzwa kwa wananchi.

"Wafugaji baada ya kuona ng'ombe wanapungua walifanya uchunguzi ndipo siku hiyo wakawakuta porini wakichuna ngozi na kuwachoma mkuki," alisema mmoja wa shuhuda.

Mwenyekiti Mbichi aliyegundua vifo vya watu hao, alisema alitoa taarifa kwa uongozi wa kata ambao walisambaza kwa mamlaka nyingine, ikiwamo Jeshi la Polisi na Idara ya Afya kwa taratibu za kiutaalamu.

Ofisa Mtendaji Kata ya Namayuni, Castro Deus, alithibitisha kutokea kwa mauaji ya Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mitopo na mjukuu wake na kwamba baada ya wauaji kutekeleza walichokikusudia waliondoka zao.

"Ni kweli tukio la mauaji kwa watu hao limetokea katika eneo langu la utawala na miili pamoja na pikipiki inayodaiwa kutumika kubeba nyama," alisema Deus.

Mganga wa zahanati ya kijiji na Kata ya Namayuni, Dk. Felster Ndanzi, aliyeifanyia uchunguzi miili ya watu hao na kutaja sababu ya kifo ni kutokwa na damu nyingi kutokana na majeraha kwenye miili yao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, John Imori, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na uchunguzi wa awali umebaini kuwa walichomwa na vitu vyenye ncha kali mgongoni na kichwani.

Aidha, alisema wanawashikilia Said Mohamedi Kilindo (33) na Seifu Abdalla Mkumbuka (57), kwa uchunguzi zaidi, huku akiwataka wananchi kujiepusha na kujichukulia sheria mkononi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Umoja unahitajika Simba sasa kurudi kwenye ramani

**KIPIGO** cha mabao 5-1 dhidi ya Yanga bado kinaendelea kuitafuna Simba kwani licha ya uongozi wa klabu hiyo kumfuta kazi Kocha Mkuu, Robertinho Oliviera na Kocha wa Viungo, Corneille Hategekimana, shinikizo sasa limehamia kwa baadhi ya viongozi kutakiwa kuachia ngazi.

Baadhi ya mashabiki na wanachama wanaamini kipigo hicho kimechangiwa na viongozi kushindwa kutekeleza vema majukumu yao, hivyo kuwataka Mwenyekiti wa Wanachama, Murtaza Mangungu na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Salum Abdullah 'Try Again', kuachia ngazi.

Wengine wameenda mbali zaidi wakidai usajili mpya uliofanywa chini ya Try Again haujakidhi mahitaji ya timu hiyo kwa kuwa ni wachezaji wawili tu ndio wameingia katika kikosi cha kwanza, Che Fondoh Malone na Fabrice Ngoma.

Lakini pia wapo wanaodai kuwa wachezaji wengi waliosajiliwa Simba umri umewatupa mkono ukilinganisha na wa watani wao wa jadi, Yanga ambao wengi ni vijana, hivyo kumtaka Try Again kuwajibika kwa kuachia ngazi.

Hata hivyo, hayo yote yanaibuka mara tu baada ya kipigo hicho kwani kabla ya hapo suala kubwa lilikuwa timu kukosa muunganiko na kushindwa kucheza soka lao la kuvutia maarufu 'pira biriani', ambalo ndio falsafa yao.

Pamoja na hayo yote, sisi tunaona, wanachama na mashabiki wa Simba wanapaswa kutambua kama ni makosa katika usajili tayari yamefanyika, hivyo hawana budi kuwavumilia wachezaji waliopo na kuwatia moyo ili kuweza kupambana msimu huu.

Ingawa tunatambua dirisha dogo la usajili litakwenda kufunguliwa mwezi ujao, ikumbukwe pia hakuna wachezaji wazuri wengi wanaopatikana sokoni katika dirisha hilo, hivyo kubwa kwa Wanasimba ni kuendelea kuwa wamoja na kuwasapoti hawa waliopo.

Na hata kama watapatikana wachezaji bora sokoni katika dirisha dogo lijalo, pia ni vigumu kufanya mabadiliko makubwa na timu kuweza kupata muunganiko mapema wakati ligi inaendelea, hivyo kikubwa ni kuwaunga mkono waliopo.

Hata hivyo, sisi bado tunaamini Simba ina wachezaji bora wanaoweza kuwapa ubingwa na kufikia malengo yao ya kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu kama wakipewa sapoti na utulivu ukitawala klabuni.


Kimatokeo uwanjani bado ina wastani mzuri wa ushindi kwani imepoteza mchezo mmoja na kutoka sare moja kati ya mechi nane ilizocheza za ligi kama ilivyo kwa Yanga lakini yenyewe ikicheza mechi tisa na kushinda nane.

Aidha, hata kama Mangungu na Try Again wakiachia ngazi hilo haliwezi kuwa suluhisho la timu kupata matokeo chanya kwani na wao kuna watu wao wanaowakubali zaidi, hivyo wanaweza kuanzisha makundi nje ya uwanja ya kuzidi kuigawa klabu na hata wachezaji.

Sisi bado hatujaona sababu ya msingi ya kufutwa kazi Robertinho ambaye tangu ametua Simba katikati ya msimu uliopita huo ulikuwa mchezo wake wa kwanza kupoteza kwenye ligi huku timu ikiwa katika nafasi nzuri ya kutimiza malengo yao ya ubingwa na kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo utulivu na umoja unahitajika hasa katika kipindi hiki kuliko kuendelea kuwanyoshea vidole Try Again na Mangungu.

Lakini pia tunayasema hayo hasa, tukitambua mechi ya 'Dabi ya Kariakoo' huwa inachezwa nje na ndani ya uwanja kisaikolojia zaidi, na anayezidiwa hupoteza, hivyo kufutwa kazi kwa Robertinho viongozi walijaribu tu kutafuta namna ya kuepusha lawama kwao jambo ambalo sasa wanapaswa kutuliza akili ya kuwaweka mashabiki na wanachama kuwa kitu kimoja hasa ikizingatiwa Novemba 25, mwaka huu wanamchezo mgumu wa kwanza wa hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Muungwana Lazima Nilonge

# Nidhamu imeigharimu JKT Queens Ligi ya Mabingwa

Na Adam Fungamwango

**KADI** nyekundu aliyoipata Happyness Mwaipaja wa JKT Queens dakika ya 29 ndiyo kwa kiasi kikubwa iliyoiangusha timu hiyo na kushindwa kwenda hatua ya nusu fainali.

JKT Queens imeshindwa kuifikia rekodi ya Simba Queens iliyoiweka msimu uliopita ilipofanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, iliyochezwa nchini Morocco na kushika nafasi ya nne. JKT Queens ambayo kwa jinsi ilivyojiandaa ikiwa na wachezaji mahiri, ilitabiriwa huenda ikaifikia hatua hiyo au kuivuka kabisa. Haikuwa hivyo, kwani juzi, ikiwa inahitaji sare tu dhidi ya, Sporting Casablanca ya Morocco, ilipokea kipigo kikali cha mabao 4-1 kwenye Uwanja wa Laurent Pokou nchini Ivory Coast.

Si kwamba ilicheza vibaya sana, hata wachezaji wawili walipokuwa wameshatolewa uwanjani kwa kadi nyekundu, bado wachezaji wa JKT Queens walionekana kupambana kisawasawa na kuwazidi kwa stamina na pumzi Wamorocco hao ambao walikuwa tayari wameshakuwa hoi bin taaban licha ya kwamba walikuwa wametimia wote 11.

Sababu iliyosababisha kufungwa mabao hayo na kutolewa ni nini? Binafsi naweza kusema ni uchezaji wa 'kisela' uliokuwa ukifanywa na baadhi ya wachezaji wa JKT Queens ndiyo uloigharimu.

Baadhi ya wachezaji walikuwa badala ya kufuata mpira na kunyang'anya kwa nguvu na maarifa, wakawa wanapandishia miguu yao kwenye ugoko wachezaji wa Morocco na kuwagonga.

Inawezekana kabisa ikawa ndiyo mchezo wao, au hucheza hivyo wanapokuwa nchini kwenye Ligi Kuu ya Wanawake, lakini wao wenyewe au makocha wao walishindwa kutahadharisha kuwa kwa sasa wanacheza michuano mikubwa ambayo inatumia Teknolojia ya Kumsaidia Mwamuzi (VAR), hivyo rafu zinaonekana kwa urahisi sana.

Mchezaji akicheza chini ya VAR anatakiwa kuwa makini sana, kwani siyo jicho la mwamuzi pekee linaloangalia, bali kuna watu wengine vyumbani ambao wanazirudia video linapotokea jambo ambalo linaonekana lina utata.

Happyness alimchezea rafu mchezaji mmoja wa Sporting Casablanca ndani ya eneo la hatari, mwamuzi akaamuru penalti tu, lakini VAR ikamkumbusha kuwa si penalti tu, bali rafu iliyochezwa ni ya kadi nyekundu.

Mwamuzi alikwenda kuangalia ili kujiridhisha na kweli, aliporudi alitoa kadi nyekundu ambayo ilionekana kuimaliza mechi yenyewe, kwani mchezaji alitoka na Meryem akapachika bao kwa mkwaju wa penalti, kilichofuata ni mfululizo wa mabao mengine ya Cheymaa Mourtaji, N'Guessan Koffi na Sylviane Adjoua, la kufutia machozi la Watanzania likiwekwa wavuni na Stumai Abdallah.

Kilichofanyika awali kilionekana tena dakika ya 85, Anastazia Simba alipopandisha tena mguu wake kwenye ugoko wa mchezaji wa timu pinzani, kwa haraka haraka mwamuzi hakuona kama ni rafu mbaya.

Lakini akaitwa kwenye VAR kujiridhisha, ikaonekana ni rafu ya kadi nyekundu. Nina uhakika, bila kadi nyekundi ya kwanza, JKT Queens ingeweza hata kushinda mechi ya juzi, achilia mbali kutoka sare.

Kinachotakiwa sasa kwa makocha wa timu hiyo ni kukaa na wachezaji wao na kuwaambia wameshakuwa wachezaji wakubwa, hivyo wanatakiwa kucheza soka la ufundi na kutumia nguvu na mwili na si kucheza 'kisela' kwa rafu zile za mitaani. Wameshatoka huko, sasa hivi wanacheza soka la kulipwa.

Wajue wamefikia kiwango cha kucheza soka huku wakiwa wanaangaliwa au kufuatiliwa na VAR, hasa wanapocheza mechi kubwa za kimataifa.

JKT Queens ilikuwa na timu bora sana kwenye michuano hiyo, lakini nidhamu imewaangusha, walimu wanatakiwa wasimamie hilo, kwani hata ukiwa na timu bora vipi, bila nidhamu ni kazi bure kama tulivyoona juzi.

HABARI KITAIFA

# Makonda ahoji TARURA kutoa kipaumbele barabara za viongozi

**Na Beatrice Shayo,** GEITA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeagiza Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), kujenga barabara kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi badala ya zinazokwenda kwenye nyumba za viongozi.

Kadhalika, kimesema kuna baadhi ya watumishi wanashirikiana na wanasiasa kutoa rushwa kwa mkandarasi kupewa tenda.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Paul Makonda, alitoa agizo hilo wakati akihutubia mkutano wa hadhara katika viwanja vya Nyankumbu, mkoani Geita.

Alisema zipo zaidi ya kilometa 17 ambazo zinaingia kwenye mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji Tanzania (TACTIC), ambazo wananchi wa Geita wamezipa kipaumbele ziende kutoa huduma kwa wananchi.

"Chama kinaelekeza mkoa uhakikishe unashirikiana vizuri na wilaya kutoa kipaumbele kwa barabara zinazoenda kwenye huduma za wananchi kwa wingi ikiwezekana kama ni eneo la soko, shule, kituo cha polisi, ama hospitali sehemu ambayo watu wote tunaitumia," alisema Makonda.

"Tusijenge barabara inayoenda kwenye nyumba ya viongozi lahasha, mimi sitaki, nataka chama kilichopo Mkoa wa Geita, kama wilaya mshirikiane na madiwani kupeleka mradi kwenye barabara zinazowahusu wananchi."

Makonda alisema kuna maeneo yana kasumba barabara inapelekwa kwanza kwa viongozi halafu wananchi wanaachwa, hilo sio sahihi kipaumbele Mkuu wa Mkoa, Martin Shigela, na timu yako ni barabara zinazowahusu wananchi.

Aidha, Makonda alisema kuna tabia mbili ambazo chama zinatakiwa kupambana nazo hasa ngazi ya wilaya na mkoa ili watumishi wasiendelee kusababisha migogoro kwa wananchi.

"Kamati za siasa za wilaya na kamati za siasa za mkoa wazishughulikie nilifarijika nilivyokuwa Dodoma kamati ya siasa ya mkoa walibaini migogoro mingi iliyosababisha tukapata kura chache Dodoma na migogoro hiyo ilisababishwa na watumishi wa ardhi walioshirikiana na wajanja wachache kudhulumu haki za wanyonge," alionya.

Alisema watu wana madukuduku yao mioyoni na kukasirika, kamati ya siasa ilifanya kazi vizuri na kuwabaini watumishi hao na kuwashughulikia.

Aidha, Makonda alizitaka kamati za siasa za wilaya na mikoa zisiwavumilie watumishi wa umma ambao ni chanzo cha migogoro.

Alisema mtumishi yeyote ambaye anakwamisha maendeleo lazima achukuliwe hatua na chama hakipo tayari kuona wananchi wananyimwa haki zao.

"Shida ya pili tuliyonayo ni rushwa jambo hili linaturudisha nyuma katika maendeleo ipo rushwa ya mkandarasi ni nani apate tenda, ipo rushwa ya mradi huu ujengwe wapi, ipo rushwa ya nani atanufaika na mradi huu ukijengwa kwenye kata yake na wapo baadhi ya watumishi wanashirikiana na wanasiasa au ni hulka yao nao wanaturudisha nyuma kwenye maendeleo," alisema Makonda na kuongeza:

"Niombe kamati za siasa za wilaya na mikoa mnayo mamlaka kwenye ilani kila mradi umeainishwa na Mwenyekiti, Rais Samia Suluhu Hassan, ametupatia fedha kazi yetu kama chama ni kufuatilia kila hatua haina picha nzuri kuona mradi umeletwa, fedha zimeletwa halafu kajanja kamoja kanakula hizo fedha."

Alisema inawezekana ujio wake umeshindikana kupata taarifa zote kwa wakati mmoja na kuwataka kuchukua hatua kwa watu wote ambao wanarudisha maendeleo nyuma.

Alisema Mwenyekiti wa chama hadaiwi, ametoa mabilioni ya fedha kazi iliyopo ni utekelezaji wa miradi.

"Nilimuuliza ndugu yangu mkataba unasainiwa lini anaanza unajua kuna siku kadhaa...kwani mlivyotafuta hela hamkujua kuna siku kadhaa? Kwanini unaanza kutafuta fedha au mpango, tukishapata fedha tunaanza kupanga kabla ya hela."

Alisema kamati za siasa za wilaya na mkoa zikiwabana vizuri watendaji na kushirikiana, miaka michache ijayo huduma za maendeleo kwa wananchi zitapatikana zote.



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ikiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. David Mathayo (wa kwanza kushoto) na Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga (wa pili kutoka kulia) baada ya kutembelea kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme cha Msamvu, mkoani Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati ya Bunge yapongeza Tanesco kukamilisha miundombinu umeme SGR

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeipongeza Wizara na Shirika la Umeme Nchini (Tanesco) kwa kukamilisha ujenzi wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa KV 220 kutoka Kinyerezi (Dar es Salaam) hadi Kingolwira (Morogoro) yenye urefu wa kilomita 160 ambayo itakuwa na umeme wa uhakika utakaolisha vituo vyote vinne vya kupoza umeme vilivyopo katika reli ya kisasa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dk. David Mathayo, alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki wakati kamati hiyo ilipotembelea kituo cha mradi huo kwa ajili ya uendeshaji wa Treni ya Mwendokasi (SGR) na kukamilisha kazi hiyo kwa asilimia mia moja.

Kamati hiyo pia, imetembelea kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Msamvu na kufurahishwa na utayari wa kituo hicho kuhudumia miundombinu kwa ajili ya treni ya mwendokasi.

Akizungumza wakati wa mkutano na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dk. David Mathayo, aliiomba serikali kutoa elimu kwa wananchi wa jirani na maeneo ya mradi ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

"Ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha mradi wa miundombinu ya mradi wa SGR. Pia tumejionea wenyewe mradi wa umeme kutoka Kinyerezi mpaka Msamvu, umekamilika kwa asilimia mia moja. Kamati tumeridhishwa sana na mradi ambao serikali imefanya," alisema.

Dk. Mthayo alisisitiza maeneo ambayo treni ya umeme imepita ni vyema serikali ikaongeza ulinzi kwa kushirikiana na serikali za mitaa kuhakikisha wananchi hawapiti katika maeneo yaliyowekewa uzio ili kuzuia ajali.

Dk. Mathayo amelihimiza Tanesco kukamilisha kazi katika maeneo machache yaliyobaki ambayo ni asilimia moja kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC) ili kukamilisha mambo yaliyobaki.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alisema Wizara ya Nishati itaongeza usimamizi kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati kwa maeneo yaliyosalia.

KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Ugomvi wa mkurugenzi, mbunge wadaiwa kukwamisha ujenzi shule

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kufanya uchunguzi kubaini kinachokwamisha kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Lipangalala, iliyopo wilyani kilombero.

Hatua hiyo inatokana na Mkuu wa mkoa kufika eneo la mradi na kutoridhishwa na kasi ya utekelezaji kunakochangiwa na ugomvi baina ya Mkurugenzi Mtendaji na Mbunge wa Jimbo la Kilombero, hali inayodaiwa kuchangia kuzorotesha maendeleo ya ujenzi wa mradi wa shule hiyo.

Serikali kuu ilitoa Sh. milioni 528, Juni 25, mwaka huu na kuingizwa katika akaunti ya shule mama ya sekondari Kiongwile.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Kilombero na kamati yake ya ulinzi na usalama pamoja na Takukuru mkoa kuanza mara moja uchunguzi wa kina ili kubaini kiini cha kukwamisha mradi huo.

Mhandisi wa ujenzi wa halmashauri aliyedaiwa kuvuruga mradi aliondolewa, lakini bado ujenzi hauendi.

"Tuliambiwa mhandisi wa wilaya ndiye anayekwamisha, tumemwondoa, na kila mtu anauliza Lipangalala mpaka sasa ujenzi unasuasua na fedha zimeshatolewa na serikali," alisema Malima.

Mkuu wa Mkoa aliuagiza uongozi wa halmashauri hiyo kukaa kama timu moja kumaliza tofauti zao na iwapo wanazo tofauti zao hilo ni jambo lingine na hataki kulijua.

Malima alishangazwa kuona halmashauri imeshindwa kukamilisha kwa wakati mradi huo, wakati wenzao wa Halmashauri ya Mlimba waliopewa fedha kwa wakati mmoja na kiwango kama hicho, tayari majengo yao yamekamilika na kupauliwa.

"Fedha imeletwa tangu Juni 25, 2023 na leo (Novemba 2023) tunakwenda zaidi ya mwezi wa tano na hatua iliyofikiwa ya ujenzi bado hairidhishi kabisa," alihoji.

Alisema, haiwezekani Mkurugenzi wa halmashauri pamoja na Mbunge wa jimbo wakawa wanabishana, halafu wananchi wanaendelea kukosa huduma, hayo ni ya kijinga na hajawahi kuyaona.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Lena Nkaya, alisema Sh. milioni 528 kutoka serikali kuu zilipokewa Juni 25, mwaka huu na kuingizwa katika Shule ya Sekondari Kiongwile kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya Lipangalala.

Nkaya alisema fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa nane, maktaba, jengo la ICT, jengo la utawala, matundu ya vyoo kwa ajili ya watoto wa kiume na wa kike ambao ulianza Oktoba mosi, mwaka huu na ulitarajiwa ukamilike Oktoba 23, mwaka huu

Nkaya alisema katika kutafuta mafundi na wazabuni, ilionekana gharama za mafundi na vifaa vilikuwa juu zaidi ya fedha iliyopokewa.

Akijitetea kwa Mkuu wa mkoa, alisema halmashauri ilipata shida upande wa wazabuni pamoja na mafundi.



Mkuu wa Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC), Aristid Kanje akizungumza na kumkaribisha mgeni rasmi Kamanda Msaidizi kutoka Jeshi la Anga la Uganda, Brigedia Jenerali Stephen Kiggundu katika mahafali ya chuo hicho mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# OUT yajivunia kutekeleza vizuri mradi wa HEET

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), kimepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa mradi wa HEET, baada ya vipengele vyote muhimu kutekelezwa kikamilifu.

HEET ni mradi wa miaka mitano kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kukuza elimu ya juu kama chachu ya uchumi mpya wa Tanzania.

Mradi huo umeundwa ili kufufua na kupanua uwezo wa vyuo vikuu kuchangia katika maeneo muhimu ya uvumbuzi, maendeleo ya kiuchumi, na umuhimu wa soko la ajira, kwa kuwekeza katika miundombinu inayohitajika kwa ufundishaji na utafiti wa kisasa na mzuri na mafunzo ya kiwango cha juu zaidi kwa walimu, watafiti na wasimamizi wanaohitajika na vyuo vikuu.

Hayo yamesemwa jana na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Taaluma, Utafiti na Ushauri elekezi Prof. Deus Ngaruko wakati akitoa ripoti ya utekelezaji kwa wativa, wakurugenzi, wakuu wa idara na vitengo vya OUT mjini Bagamoyo mkoa wa Pwani.

Kikao kazi hicho cha siku mbili juzi na jana kimewaleta pamoja wataalam mbalimbali.

"Kimsingi, OUT imepiga hatua kubwa sana katika utekelezaji wa mradi wa HEET na ninyi nyote kama viongozi wa chuo mnapaswa kufahamu na kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa mradi hatua kwa hatua ili pale tunapopata changamoto tunaitatua kwa pamoja.

Kwa mujibu wa Profesa Ngaruko ambaye pia ni Mratibu Mkuu wa mradi wa HEET: "Hakika haya ni mafanikio makubwa na sasa tuendelee kufanya kazi kwa kushirikiana ili utekelezaji wa mradi ukamilike kwa wakati."

Alisema OUT kupitia ufadhili wa serikali chini ya Benki ya Dunia kupitia usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inayosimamia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya kiuchumi nchini (HEET).

Alisema OUT kimekuja pia na mradi wa uwekezaji wa kituo cha Utafiti, Ubunifu na Ugundizi (ORIC) kitachojengwa mjini Kibaha ambacho kitasheheni viwanda, mashamba, mabwawa ya samaki na utakatishaji majitaka, mifugo, majiko na maabara za kisasa za sayansi na utalii zitakazotumiwa katika tafiti na mafunzo kwa vitendo.

"Wanafunzi wa mazoezi kwa vitendo, kazi za kujitolea na wasio na uwezo wa kujilipia ada watafanya kazi za uendeshaji wa kituo na kupata kipato kitakachowasaidia kimasomo. Wabobezi na wanasayansi kutoka taasisi ngingine za ndani na nje ya nchi pia watakaribishwa kutumia kituo hicho kwenye kazi zao za kitaaluma na kiutafiti." Alisema Prof. Ngaruko.

Naibu Mratibu wa mradi, Dk. Timoth Lyanga, akitoa taarifa za utekelezaji wa mradi wa HEET alisema mradi unaendelea vyema na sasa kinachofanyika ni kuhitinishwa kwa zoezi la tathmini za kimazingira na masuala ya kijamii (ESIA) na wakati huo huo mchakato wa kuwapata wakandarasi watakaojenga majengo ya maabara saba za kikanda likiwa linaendelea vyema.

Kwa upande wake mratibu wa mradi katika kipengele cha kuwaendeleza wanataaluma na upitiaji wa mitaala, Dk. Yohana Lawi, alisema bado nafasi moja imebaki kwa wanataaluma kwenda masomoni na nafasi nyingine zote zimeshajaa.

Kwa upande wa mitaala kazi mbili kubwa tayari zimekamilika ambazo ni kuwatafuta wahitimu na mahitaji ya soko, na kwamba kazi inayoendelea sasa ni idara na vitivo kuitisha mikutano ya wadau na kisha kuwasilisha mitaala husika kwenye vyombo vya maamuzi katika ngazi ya chuo.

Mradi wa HEET unatoa ufadhili kwa wasichana na wanawake 1,000 wenye sifa za kujiunga na mafunzo ya awali ya msingi kwa mchepuo ya sayansi, injinia, teknolojia na hesabu waliopitia changamoto mbalimbali zikiwemo kupata ujauzito, umasikini, ukatili wa kijinsia na changamoto za maisha zilizosababisha wakatishe masomo yao.

# Vituo vya kulea watoto yatima vyapewa angalizo

**Na Sabato Kasika**

WAMILIKI wa mashirika binafsi yenye vituo vya kulea yatima na watoto wanaoishi mazingira magumu, wametakiwa kufuata utaratibu na miongozo ya serikali wa kuwalea watoto hao.

Malekezo hayo yalitolewa na Ofisa Ustawi wa Jamii wa Hospitali ya Rufani Mwananyamala, jijini Dar es Salaam, Asia Mkini.

Alisema hayo wakati akipokea msaada wa vitu mbalimbali zikiwamo sabuni na mafuta, vilivyotolewa na taasisi ya Eden Twins Foundation, kwa ajili ya kinamama waliojifungua mapacha Novemba 11, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mapacha.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Diana Mbena, alisema kuwa wapo baadhi ya wamiliki wa mashirika wanafuata wazazi na walezi, hasa wenye watoto mapacha ambao hali yao ya kiuchumi ni ngumu na kuwaomba wawape watoto wakawalee.

Diana alisema hakubaliani na utaratibu huo, kwa kuwa unalenga kuwanufaisha wenye mashirika, huku wenye watoto wakiendelea kubaki maskini

Alisema ni muhimu watu wa aina hiyo wafuate utaratibu wa kupeleka maombi ustawi wa jamii badala ya kuchukua kienyeji.

"Wanapopeleka maombi ni lazima ustawi wa jamii nao wajiridhishe ni wapi mtoto anapelekwa na ataishi mazingira ya aina gani," alisema Asia.

Alisema hairuhusiwi mtu kuchukua au kumtoa mtoto kienyeji ni lazima utaratibu ufuatwe, kinyume na hapo ni kutaka kujinufaisha.

Alisema wazazi au walezi wasikubali kugawa watoto wao, na kama ni magumu waende katika ofisi za ustawi wa jamii zilizo karibu yao kupata ushauri na maelekezo.

"Haturuhusu mtoto achukuliwe kwenda kokote bila kufuata utaratibu unaoeleweka, hivyo niwaombe enyi Eden Twins Foundation mtusaidie kuendelea kuwaweka wazi hao wanaopita mitaani kuchukua watoto," alisema.

Awali, akielezea msaada ambao taasisi yake imetoa, alisema imetembelea hospitali nne za Temeke, Ilala, Muhimbili na Mwananyamala.


"Tumekabidhi nguo za watoto, sabuni za kuogea na kufulia, mafuta ya kupaka, maziwa, pampasi, vyote jumla vikiwa na thamani ya Shilingi milioni mbili," alisema Diana.

Alisema Novemba 11 kila mwaka wameitenga kama siku ya mapacha ambayo wanaiadhimisha kwa kuwasaidia kwa hali na mali wazazi wenye mapacha wenye hali ngumu ya kiuchumi.

"Sio kwamba wote wanaozaa mapacha wana hali ngumu, lakini ukweli ni kwamba wengi wao wanaishi maisha ya shida, ndio maana nikaanzisha taasisi hii ili kujaribu kuwasaidia," alisema.

Aliomba wazazi wenye mapacha ambao hali za kiuchumi ni duni, watambuliwe kama kundi maalum linalohitaji kusaidiwa.

"Ninaomba hivyo, kwa sababu wapo ambao wamekimbiwa na waume zao, kwa madai kuzaa mapacha ni laana au sababu nyingine zisizo za msingi. Wengi wao wanaishi maisha magumu wanahitaji kusaidiwa, mimi peke yangu siwezi ndio maana ninaomba kundi hili litambuliwe kama kundi maalum," alisema.



# TAWIRI: Simba waongezeka kwenye hifadhi za taifa nchini

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

IDADI ya Simba katika Hifadhi za Taifa Tanzania imeongezeka kufikia 17,000. Imeelezwa.

Ongezeko hilo linaifanya Tanzania kwa sasa kuwa kinara katika mataifa yenye wanyamapori hao wengi zaidi duniani.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, (TAWIRI), Dk. Ernest Mjingo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifafanua jambo kwa waandishi wa habari kuelekea kongamano la 14 la wanasayansi wa wanyamapori katika nchi 20 duniani. Kongamano la wanasayansi hao litafanyika mwezi Desemba mwaka huu Jijini Arusha. Tanzania ina jumla ya hifadhi 22 zinazosimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

"Taarifa za kuongezeka kwa simba tunaendelea kuzichakata. Mafanikio haya makubwa ya kujua idadi ya simba yametokana na kazi kubwa iliyofanywa na jopo la watafiti wa TAWIRI na wahifadhi kutoka taasisi nyingine za hifadhi.

"Matokeo kamili ya idadi ya Simba na wanyama wengine yatatolewa rasmi na Waziri mwenye dhamana katika kongamano hilo la kimataifa."

Kwa mujibu wa Dk. Mjingo, TAWIRI baada ya kumaliza utafiti huo, kwa sasa inajua idadi ya wanyama wote nchini na wapi wanapatikana.

"Nia ya utafiti huu ni kusaidia mamlaka zinazohusika na watalii, kuwezesha kufikisha matarajio ya wageni kufanya utalii.

"Ndio maana tunasisitiza kwenye mikutano yetu ya matokeo ya utafiti kama huu wa wanasayansi, wadau wa uhifadhi na wenye kampuni za kuongoza watalii, washiriki maana utafiti wetu unaelekeza vivutio vilipo, kwa kiasi gani na wakati gani vinapatikana," alisema Dk. Mjingo.

Kuhusu mada zitakazowasilishwa na kujadiliwa katika kongamano hilo, alisema ni pamoja na athari za magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyamapori kwenda kwa binadamu, mimea vamizi na migongano ya wanyamapori na binadamu.

"Zaidi ya asilimia 75 ya magonjwa yanayoathiri binadamu yanaambukizwa kutoka kwa wanyamapori na wanyama wafugwao. Yote haya yatajadiliwa na wanasayansi ili kuona namna ya kudhibiti na huku uhifadhi na maisha yakiendelea"alisema.

Aidha, Mkurugenzi wa Utafiti wa Wanyamapori wa TAWIRI, Dk. Keyu, alisema utafiti wa hivi karibuni uliofanyika, umefanikisha kugundua aina mpya za vipepeo, nyoka na nyani.

Alitaja aina mpya ya vipepeo wanaovutia kwa macho ni 'Caracrase mtuyae' ambaye amegunduliwa katika Bonde la Kihansi, wakati nyoka mpya mwenye pembe mbili kichwani aligunduliwa katika Hifadhi ya Taifa Udzungwa.

Vilevile, Dk. Keyu, alisema aina mpya ya nyani aliyepewa jina la 'Kipunji' amegundulika katika Milima ya Rungwe na Milima ya Livingstone.

Dk. Keyu, alisema viumbe hao wapya kugunduliwa nchini, wataongeza idadi ya vivutio, ambavyo watalii na watafiti watapenda kuja kuviona na hivyo kuongeza idadi ya watalii.

TAWIRI, ni taasisi ya umma iliyoko chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge, Namba 4 ya Mwaka 1980.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella (kushoto) akimsikiliza Meneja wa Kanda ya Kaskazini wa Dar Ceramica Centre, Irene Lyimo wakati wa uzinduzi upya wa Tawi la kampuni hiyo la Arusha. Kulia ni Mkuu wa Mauzo na Masoko, Raymond Nkya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge la vijana Afrika Mashariki lataka lugha moja nchi wanachama

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

BUNGE la Vijana la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAYLA), limependekeza wakuu wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo (EAC), kuja na lugha moja, itakayotumika katika mawasiliano ya utangamano kwa nchi zote, ili kuondoa mkanganyiko wa matumizi ya lugha kuu.

Hoja ya kutaka kuwapo kwa lugha moja, iliibuliwa juzi katika mkutano wa EAYLA, uliofanyika Jijini Arusha.

Brian Odero (Kenya), ambaye ni Spika wa zamani wa Bunge hilo la vijana, alisema mojawapo ya vikwazo katika jumuiya hiyo kwa sasa, ni kukosekana kwa lugha moja kuu ya kuziunganisha nchi wanachama.

"Kenya hatuko vizuri katika kiswahili, lakini pia hata wenzetu Uganda, siyo kwamba wanazungumza kiswahili kizuri.

"Tuko jumuiya moja, natamani tuwe na lugha moja ambayo ni Kiswahili na kifundishwe kwa nchi zote wanachama ili tuweze kuzungumza lugha moja,"alipendekeza Odero.

Alisema ziko tetesi kuwa Eritrea, Somalia na Ethiopia, wameomba kujiunga na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, lakini kila nchi na lugha yake.

Mratibu wa Bunge hilo, Abdillah Lugome, alisema vijana wanatakiwa kujadili namna gani kutakuwa na sarafu moja ya jumuiya hiyo, pamoja na kuondoa vikwazo kwa vijana kuingia katika nchi wanachama, bila kuwa na visa.

"Mfano mzuri, tunaona kwa Rais, Paul Kagame, ameruhusu nchi wanachama wa EAC, kuingia Rwanda bila masharti ya kuwa na hati za kusafiria. Tunatamani na nchi nyingine zote kuwa hivyo ili kurahisisha wanachama kufanya shughuli za maendeleo bila vikwazo,"alisema Lugome.

Aidha, Katibu wa Bunge hilo, Caroline Manyama (Tanzania), alisema katika muhula huu waliopewa kama viongozi, watahakikisha kuwa vijana wanapewa vipaumbele katika kuleta maendeleo ya Jumuiya hiyo.

Spika wa Bunge hilo la vijana la EAYLA, Amanya Belinda (Uganda) alisema Bunge hilo litatoa ushirikiano wote unaohitajika katika kuhakikisha vijana wanashirikishwa kikamilifu katika ujenzi wa Afrika Mashariki.

Wakati anafungua mkutano huo, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Joseph Ntakarutimana, alisema watafanya jitihada zote kuwasapoti vijana, kwa kuwa vijana wana nguvu ya kuleta mabadiliko chanya katika kuboresha utangamano na maendeleo ndani ya jumuiya hiyo.

# NECTA kunoa walimu utungaji bora mitihani

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAKATI Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), likielekea kuadhimisha miaka 50 ya kuanzishwa kwake, limesema linakusudia kuanza kutoa mafunzo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari, juu ya namna bora ya utungaji wa mitihani ya umahiri, baada ya mitaala kubadilishwa.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Said Ali Mohamed, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati alipokutana na walimu wa taaluma 180 Jijini Tanga.

Kati ya walimu hao, 107 ni walimu wa shule za msingi na walimu 73 ni sekondari.

Katibu huyo, alisema kupitia mabadiliko makubwa ya sera ya elimu yanayokuja, NECTA imeanza kujiandaa kutoa mafunzo kwa walimu wa taaluma, kwa kuwa wao ndiyo viongozi wa taaluma katika shule, hivyo watakapopatiwa mafunzo hayo watawezesha walimu wenzao.

"Katika kuelekea maadhimisho haya kuna mambo mbalimbali tumeyafanya, tumekwisha na tunaendelea kuratibu zoezi la upandaji miti kwa sababu NECTA imekuwa mtumiaji mkubwa wa karatasi, lakini pia tuko hapa kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya namna bora ya kutunga maswali ya mitihani," alisema.

"Tunafahamu kuwa tuna mitaala inayopelekea kutunga maswali ya umahiri, lakini pamoja na hilo tuna mabadiliko makubwa yanayokuja ya sera ya elimu na haya ndiyo tumeanza kuyatekeleza" alifafanua Mohamed.

Aidha, Katibu huyo alisisitiza kuwa katika mwendelezo huo, NECTA imeshatoa mafunzo kwa walimu wa sayansi na wataalamu wa maabara 21,000 na mafunzo ya upimaji kwa njia ya umahiri, kwa walimu 16,000.

Katika mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, alitoa wito kwa walimu hao kuyaishi mafunzo wanayopatiwa.

Aidha, alitoa wito kwa walimu hao kutumia fursa hiyo ya mafunzo, ili wakatoe elimu kwa wengine ambao hawakupata bahati ya kuhudhuria na kuongeza kwamba serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeboresha mazingira ya elimu.

"Mafunzo mnayopatiwa hapa mwende mkayafanyie kazi, na mimi nataka walimu Mkoa wa Tanga mtembee kifua mbele kwakuwa ninyi ndiyo walezi wa watoto wakiwa shuleni, na nina imani ndani ya miaka miwili hadi mitatu ijayo mkoa utabadilika na kuwa na maendeleo makubwa kwani mazingira ya elimu yameboreshwa," alibainisha.

Wakizungumza baada ya mafunzo hayo baadhi ya walimu akiwamo Mwalimu Daud Mkulago wa Shule ya Indian Ocean English Medium ya Jijini Tanga, alisema:

"Ukiangalia mitaala yetu ilibadilishwa tangu mwaka 2014, lakini walimu bado walikuwa hawajawezeshwa namna bora ya kutunga mitihani. Sasa hivi kila kitu kimebadilika, kumpima mwanafunzi ni kumuandaa vizuri kama mwalimu hajaandaliwa inakuwa shida kumuandaa mwanafunzi."





# TAFIRI yateketeza dhana za uvuvi haramu

**Na Mathias Marwa,** MARA

TAASISI ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), kupitia mradi jumuishi wa jamii katika usimamizi wa uvuvi kwenye ardhioevu ya Mara imeteketeza nyavu za uvuvi haramu zilizosalimishwa na wavuvi zaidi ya 51 kutoka wilayani Rorya mkoani hapa na kukabidhiwa nyavu halali kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uvuvi.

Uteketezaji wa nyavu hizo pamoja na utolewaji wa nyavu halali umeongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Juma Chikota, chini ya usimamizi wa TAFIRI, Mkoa wa Mwanza kwa ufadhili wa Shirika la Darwin Initiative la Uingereza kwa lengo la kuimarisha uhifadhi wa ardhioevu ya Mto Mara.

Akizungumza juzi wakati wa hafla hiyo iliyowakutanisha wadau mbalimbali wa ulinzi wa rasilimali za Mto Mara, Mkurugenzi wa kituo cha TAFIRI-Mwanza, Dk. Baraka Sekadende, alisema dhana hizo halali za uvuvi zimegharimu zaidi ya Sh. milioni 14.6.

"Baada ya kubaini kuwapo kwa shughuli za uvuvi haramu uliokithiri kwa kushirikiana na wafadhili wa mradi huu Darwin Initiative tukaanza kampeni iliyoenda sambamba na utolewaji wa elimu juu ya madhara ya uvuvi haramu na kufanikiwa kupata idadi hii ya wavuvi waliorejesha nyavu zao na kukabidhiwa mpya ambazo ni halali," alisema, Dk. Sekadende.

Aidha, alisema licha ya kampeni bado wapo wavuvi wengine ambao wamekaidi kusalimisha nyavu haramu kwa kuogopa kuwa endapo wakizisalimisha watakamatwa dhana ambayo sio ya kweli.

Kadhalika alisema ardhi oevu ya Bonde la Mto Mara lenye ukubwa wa kilometa 387 za mraba inahitaji kuitunza na kuilinda kutokana na miongoni mwa ardhi oevu kubwa kusini mwa jangwa la Sahara.

Mkuu wa wilaya hiyo, Juma Chikoka alitoa siku 14 kwa wavuvi wote wanaojihusisha na shughuli za uvuvi haramu husususani ambao hawakusalimisha dhana zao kuzisalimisha kwa hiari kabla ya hatua kali za kisheria.

Aidha, alimuagiza Ofisa Uvuvi wa wilaya hiyo kuandaa vikao na wavuvi wote ili kuwaelimisha madhara ya uvuvi haramu pamoja na fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali ikiwamo mikopo ya serikali kuu ili kufanya uvuvi kuwa na maslahi.

Ofisa Uvuvi Wilaya ya Rorya, Godfrey Bwathondi, alisema upande wa wilaya hiyo mto huo una wavuvi 668 na 340 wanatumia zana haramu za uvuvi hivyo kuomba wadau kuendelea kushirikiana na serikali kudhibiti vitendo hivyo.

"Hizi dhana zinauzwa hadi hapa kijijini kwa bei nafuu sasa ni vyema serikali kuanzia ngazi za vijiji hadi wilaya kuweka jitihada kudhibiti na kutokomeza biashara hii ili dhana hizi zisipatikane kabisa," alisema Maendeka John, mmoja wa wavuvi.



Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Juma Chikota (mwenye suti ya bluu) akiongoza shughuli ya uteketezaji wa zana za uvuvi haramu zilizokuwa zikitumika katika ardhi oevu ya Mto Mara na kusalimishwa kwa hiari hivi karibuni na wavuvi zaidi ya 50 katika kijiji cha Kwibuse wilayani Rorya. **PICHA: MATHIAS MARWA**

# TCRA yahimiza maombi ya leseni kwa njia ya mtandao

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kupitia kwa Meneja wa Kanda ya Ziwa, Mhandisi Francis Mihayo, imewasisitiza wadau mbalimbali wa mawasiliano kufanya shughuli za usajili na maombi ya leseni kupitia njia ya mtandao lengo likiwa ni huduma ya mawasiliano iwafikie watu wengi nchini.

Mihayo alisema TCRA imejizatiti kuondoa kero ya upotevu wa muda ambayo ilimkabili mwombaji mpya na mwenye leseni ya kutoa huduma za mawasiliano hapo awali.

"Kwa sasa ikiwa unahitaji leseni ya kutoa huduma za mawasiliano kama vile kusafirisha vifurushi na vipeto, kufanya shughuli za uandishi wa habari kwenye mtandao, kutoa huduma za mtandao, anayetoa huduma za usalama mtandaoni, utangazaji wa kijamii, na nyingine zote, leseni sasa unaweza kuomba kupitia jukwaa letu la kimtandao liitwalo Tanzanite portal," alisema.

Mhandisi Mihayo alisema lengo la Mamlaka hiyo ni kufanya huduma kuwa rahisi kwa wawekezaji wote kwenye sekta ya mawasiliano, kutoka wadogo hadi wakubwa, kupata leseni kwa haraka na urahisi kupitia mfumo huo unaopatikana kwenye tovuti ya Mamlaka hiyo.

Alisema jukwaa hilo la mtandaoni linawawezesha waombaji wa leseni kuwasilisha maombi yao mapya, kuhuisha leseni zilizopo, na pia kurahisisha mchakato wa kutoa mrejesho kwa TCRA.

"Mbali na kuomba leseni mfumo huu unamwezesha mwenye leseni kupata mrejesho, kubadili umiliki, kuwasilisha na kupokea taarifa kwa TCRA, na kuipata leseni yake papohapo," aliongeza.

Alisisitiza kuwa hatua hiyo ni sehemu ya jitihada za kukuza sekta ya mawasiliano nchini na kuwahakikishia wawekezaji kwamba serikali inazingatia mazingira rafiki ya biashara.

"Ni muhimu wale ndugu zangu wanaosafirisha abiria wakakumbuka kwamba kusafirisha vifurushi au vipeto kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine bila kuwa na leseni ya kiposta inayotolewa na TCRA ni kwenda kinyume na sheria, hii ni kwa mizigo inayoagizwa."

# Mpango kuwawezesha makandarasi wazawa waiva

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imesema ipo katika mkakati wa kuwawezesha makandarasi wazawa kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kuhakikisha wanashiriki katika miradi ya ujenzi na kuitekeleza katika ubora unaohitajika.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa baada ya kufungua mkutano wa sita wa ushirikiano kati ya SJMT na SMZ katika sekta ya ujenzi na kueleza kuwa tayari serikali imeanza taratibu za kuunda timu ya pamoja ya kufanikisha mkakati huo wa kuwajengea uwezo makandarasi wazawa.

"Mpango unaenda sambamba na kuunganisha makandarasi wazawa wa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara lengo likiwa ni kuwasaidia wajenge uwezo wa kujenga barabara bila kushusha viwango vya ujenzi na huu mpango utakuwa sio wa mwaka mmoja bali miaka mingi na kila mwaka tunakuwa na vipaumbe vya kutekeleza," alisema Waziri Bashungwa.

Mkutano huo ulikutanisha watumishi mbalimbali kutoka Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi, Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ya Zanzibar mwishoni mwa wiki mkoani hapa.

Bashungwa aliwahakikishia watumishi wa pande zote mbili ushirikiano na kwamba lengo la serikali ni kuhakikisha shughuli za ujenzi na utekelezaji wa miundombinu zinafanyika kwa ufanisi pande zote mbili.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kutoka Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema awali zilikuwapo kero na hoja mbalimbali za kimuungano, lakini kutokana na mikutano na vikao mbalimbali kero hizo zimefanyiwa kazi na kurahisisha shughuli za kiutendaji katika sekta mbalimbali za pande zote.

"Wakati tunaanza vikao hivi kwa mara ya kwanza tulikuwa na hoja zaidi ya 27 wakati huo zikiitwa kero za muungano, lakini kwa sasa tumebakiza hoja tano tu na hakuna malalamiko hii ni kwa sababu ya vikao na utekelezaji wa maagizo," alisema Dk. Salum.

Awali, akitoa taarifa ya vikao vya ushirikiano baina ya serikali hizo kupitia sekta ya ujenzi, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Balozi Aisha Amour alisema vimesaidia kusainiwa kwa hati mbili za Muungano katika masuala ya ujenzi pamoja na hati nne zilizopo katika hatua za mwisho wa maandalizi kuelekea kusainiwa lengo likiwa ni kudumisha maendeleo katika miundombinu.

Nipashe
Spotika



MAKOCHA WATANO BORA SOKA LA DUNIA KWA SASA UK. 12-13




RICE

# VIUNGO WA3 BORA EPL HADI SASA MSIMU HUU

**LONDON,** England

KIUNGO wa kati inawezekana kabisa kuwa sehemu muhimu zaidi ya timu ya soka. Kwa hiyo, viungo huwa ni baadhi ya wachezaji muhimu katika upangaji wa timu.

Ligi Kuu England (EPL), inaendelea vizuri sasa, na baadhi ya viungo bora zaidi duniani wanaendelea na biashara hiyo.

Kumekuwa na viungo wachache ambao wamefanya vizuri kwenye Ligi Kuu hiyo hadi sasa msimu huu, na katika makala haya, tutajadili wachezaji watatu wa aina hiyo. Kwa urahisi, tumechagua namba sita, nane na 10 ili kuunda orodha ya utatu.

Hawa ni wale waliofanya vizuri zaidi kwenye ligi hiyo hadi sasa msimu huu, twende sasa...

**#1. Rice Declan**

Arsenal ilimsajili Declan Rice kutoka West Ham United kwa kiasi kikubwa cha fedha mwanzoni mwa msimu na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, bado hajawakatisha tamaa mashabiki wa 'Washikabunduki' hao hadi sasa. Rice amefunga mabao kadhaa na kusajili pasi ya mabao, lakini muhimu zaidi ni kuwapa safu ya kiungo ya Arsenal uhakika waliouhitaji sana.

Mabao ya Rice yaliipa ushindi Arsenal dhidi ya Manchester United na kisha kusaidia Arsenal kupata pointi dhidi ya Chelsea. Jorginho akiwa upande wake katika mechi chache zilizopita, Rice amekuwa na leseni ya kushambulia kwa uhuru zaidi katika mechi chache zilizopita, na ameonekana kustarehe kufanya hivyo.

Iwapo Arsenal wanataka kuwa katika mvutano mkali wa kutwaa taji na pia kuingia ndani kabisa ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Rice atalazimika kuwa katika hali nzuri na kutekeleza majukumu yake kwa ustadi kama anavyofanya hivi sasa.

**#2. Dominik Szoboszlai**

Safu yote ya kiungo ya Liverpool ilifanyiwa marekebisho mwanzoni mwa msimu, na Dominik Szoboszlai alikuwa mmoja wa wachezaji wengi wapya waliosajiliwa.

Si wanasoka wengi wa Hungary ambao wamefanya vema katika Ligi ya England kabla yake, na hivyo basi, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amekuwa kwenye kiwango bora kwa sasa.

Amekuwa sehemu ya ndani ya timu ya kocha Jurgen Klopp, akicheza nafasi ya namba nane. Ameonekana kustarehe kwenda mbele na pia alifunga mabao kadhaa. Pia alilazimika kuchukua nafasi ya winga wa kushoto katika mechi chache baada ya mabadiliko kufanywa katika mechi hizo.

Hata hivyo, uwezo wake wa kushinda mpira nyuma ndani ya nusu yake pia umeonekana katika mechi chache zilizopita. Huku Alexis Mac Allister akicheza kama namba sita, 'Wekundu' hao walihitaji kiungo wa kati wa eneo la boksi katika timu yao na sasa wanaonekana wamempata Szoboszlai.

**#3. James Maddison**

James Maddison labda ndiye mchezaji bora zaidi kwenye ligi, na hayo ni mafanikio fulani. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ameibuka kama mchezaji bora wa Tottenham Hotspur na pengine ndiyo sababu kuu kwa nini timu yake iko kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu baada ya mechi tisa.

Pia, amejidhihirisha kuwa ni mfungaji hodari wa timu yake. Ana mabao matatu na asisti tano katika mechi tisa za ligi, ambayo ni urejesho mzuri kwa kiwango chochote. Pia ameunda ushirikiano mzuri sana na Son Heung-min ambao umesumbua timu nyingi hadi sasa.

Maddison ni mpiga pasi mahiri, na uwezo wake wa kupata wachezaji wenzake ndani ya tatu ya mwisho kwa pasi zenye inchi nzuri unabaki kuwa muhimu kwa Tottenham.


Timu hiyo ya kocha, Ange Postecoglou haitataka kutupa mwanzo mzuri wa msimu, na Maddison anabakia kuwa katikati ya mpango wao wa kuwa na uwezo wa kusukuma mashambulizi mbele kwenye taji la ligi. Inabakia kuonekana kama Maddison anaweza kuendelea kutoa kwa upande wake.

## ISIKUPITE

MABAO mawili aliyofunga Harry Kane Jumamosi usiku wakati Bayern Munich ikishinda 4-2 dhidi ya Heidenheim, yanamfanya nahodha huyo wa England kuweka rekodi mpya Bundesliga ya kufikisha mabao 17 kwenye mechi 11 za mwanzo tangu ajiunge na timu hiyo. Hivyo ameipiku rekodi ya Robert Lewandowski aliyoiweka mwaka 2019 ya kufunga mabao 16 kwenye michezo 11 ya mwanzo alipotua Bayern.



## Extra Time



GUARDIOLA




# MAKOCHA WATANO BORA SOKA LA DUNIA KWA SASA

**LONDON,** England

KATIKA soka la kisasa, kocha hubeba jukumu lenye vipengele vingi ambalo huenda zaidi ya uwezo wao wa kimbinu. Wanafanya kazi katika mazingira ya shinikizo la hali ya juu pamoja na kuunda mikakati ya mchezo, pia wana jukumu la kupanga uwiano wa timu na ari.

**Mara kwa mara wanakabiliwa na matukio ya hali ya juu na maamuzi yao yanaweza kushawishi matokeo ya mechi au mwelekeo wa msimu. Kuwa mahiri kimbinu haitoshi kwani makocha pia wanahitaji kutafuta njia za kuwajengea wachezaji mawazo ya ushindi ili kuendeleza mafanikio.**

Kocha hatimaye ndiye mtu mkuu katika klabu yoyote ya soka. Wanabuni njia ya klabu kwenda kileleni huku pia wakiweka ari ya juu na kufanya kilicho bora zaidi kutokana na rasilimali zinazopatikana kwao.

Katika makala haya inawaangalia makocha watano bora katika soka la dunia kwa sasa...

### #5 Jurgen Klopp

Jurgen Klopp alivumilia msimu wa usiosahaulika wa 2022-23 akiwa na Liverpool. Hata hivyo, itakuwa rahisi kumtathmini kocha huyu ambaye amepata mengi katika miaka ya hivi karibuni katika msimu wake mbaya zaidi. Klopp amefanya kazi nzuri sana Liverpool katika kipindi cha miaka nane iliyopita.

Ingawa baadhi ya makocha wenzake wamekuwa na utajiri mwingi wa rasilimali ya wachezaji, kocha huyo wa Ujerumani amelazimika kufanya kazi na rasilimali chache. Bado aliweza kuunda timu ambayo ilishinda mataji yote makubwa. Klopp pia ameweza kubadilisha wachezaji wasiojulikana sana hadi kuwa nyota kwa kipindi ambacho amekuwa pale kwenye dimba Anfield.

Yeye ni kocha mahiri ambaye mtindo wake wa uchezaji una sifa ya uchezaji wa hali ya juu, mabadiliko ya haraka na ustadi wa kushambulia. Zaidi ya hayo, Klopp pia ni kocha bora na wachezaji wako tayari kutoa yote yao uwanjani kwa ajili yake.

### #4 Mikel Arteta

Mikel Arteta aliwanyamazisha wakosoaji wake na Arsenal wakawanyamazisha waliokuwa na shaka na maonesho yao ya kuvutia kwenye Ligi Kuu England msimu uliopita. Labda hiyo ndiyo sababu pia Arteta anastahili kupewa maua yake. Hakuna aliyetarajia 'Washikabundu' hao kuwa bora kama walivyokuwa msimu uliopita.

Kwani, walikuwa wamevumilia mwisho mbaya wa msimu wa Ligi Kuu wa 2021-22, wakimaliza nje ya nne bora na kushindwa kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini walirejea kwa kustaajabisha muhula uliopita, wakicheza soka ya kushambulia kwa kumiliki mpira na mchezo ambao haukuwapo hapo Emirates kwa muda mrefu.

Arteta alifanikiwa kupata wachezaji wake wote kwenye ukurasa mmoja na Arsenal walikaa kileleni mwa jedwali la Ligi Kuu England kwa siku 248 katika msimu wa 2022-23. Kwa bahati mbaya, walisalimu amri katika kipindi cha mwisho cha kampeni na wakachapwa na Manchester City ambao walibeba taji la ligi.

Lakini Arteta anapendekezwa kujumuika katika uchezaji wao kuanzia muhula uliopita na kuwapeleka Arsenal katika viwango vipya katika siku za usoni.

### #3 Carlo Ancelotti

Katika kazi yake yote ya ukocha, Carlo Ancelotti amekuwa akizingatiwa sana kwa ustadi wake wa busara na kubadilika. Daima akitikisa hali ya utulivu, kocha huyo wa Italia ana uwezo wa kipekee wa kusimamia vikosi vilivyojaa nyota huku akiendeleza hali ya utulivu katika chumba cha kubadilishia nguo.

Ancelotti ameonesha uwezo wake wa kutumia mbinu mbalimbali kwa kupata mafanikio akiwa na klabu mbalimbali. Anapima sifa za wachezaji wake na kikosi chake na mikakati ili kuendana na uwezo wao. Ancelotti aliiongoza Real Madrid kutwaa mataji ya LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2021-22.

Ndiye kocha aliyepambwa zaidi katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa ameshinda taji hilo mara nne kama kocha.

### #2 Sarina Wiegman

Kocha wa Timu ya Taifa ya Wanawake ya England, Sarina Wiegman, amekuwa mmoja wa makocha wanaotafutwa sana duniani baada ya Kombe la Dunia la FIFA la Wanawake 2023. Ingawa England iliangukia kwa Hispania katika fainali hizo, sifa za Wiegman kama mmoja wa makocha bora zaidi duniani ziliachwa bila dosari.

Mchuano wa Kombe la Dunia dhidi ya Hispania uliwakilisha fainali ya nne mfululizo ya Wiegman ya kimataifa ya wanawake. Alifika fainali zake mbili za kwanza za mashindano makubwa mfululizo akiwa na timu ya wanawake ya Uholanzi. Wiegman kisha alichukuwa jukumu la kuinoa Timu ya Wanawake ya England mnamo 2021 na amerudia mafanikio yake.

Ametinga fainali ya Kombe la Dunia la FIFA la Wanawake mara mbili na kushinda UEFA kwa Wanawake mara mbili pia. Timu zake zimesifiwa mara kwa mara si tu kwa ufanisi wao katika mashindano ya mataji, lakini pia kwa uchezaji wao wa kuvutia.

Wiegman kwa sasa anahusishwa na timu ya soka ya wanaume ya Uholanzi. Zaidi ya hayo, anaripotiwa kuzingatiwa kuwa mgombeaji mkuu kuchukua jukumu la kuinoa timu ya soka ya Wanaume ya England wakati wowote Gareth Southgate atakapojiuzulu.

### #1 Pep Guardiola

Pep Guardiola anaonesha kipaji cha usimamizi katika soka la kisasa. Anachukuliwa sana kama mtu mwenye maono ambaye anachanganya akili ya busara na mawazo ya kibunifu. Kwa kufanya hivyo, amekuwa na jukumu la kuleta mapinduzi katika mandhari ya mchezo huo mzuri.

Guardiola mara kwa mara huwavutia wachezaji wake bora na pia huunda timu zinazocheza kandanda ya kumiliki mpira huku akiwa mahiri sana katika kushambulia. Kocha huyo wa Hispania amejishindia medali nyingi katika maisha yake ya ukocha.

Kuiongoza Manchester City kutwaa mataji matatu ya msimu wa 2022-23 bila shaka ni mafanikio yake makubwa zaidi. Ingawa amebarikiwa na rasilimali nyingi, inabidi apewe sifa kwa kuzitumia kwa busara na kuhakikisha matokeo yanatolewa uwanjani.

## Nukuu

"Ningependa kumuona Bernardo Silva akiwa Arsenal. Arsenal inahitaji mchezaji kama yeye - ambaye anaweza kucheza katika kila nafasi. Unajua atacheza vizuri hata kama utamshika wapi. Pasi zake ni nzuri na ana akili sana kimbinu. Yeye pia ni mkamilifu katika chumba cha kubadilishia! Anaweza kufanya mambo mengi sana uwanjani," **Nyota wa zamani wa Arsenal, Emmanuel Petit, akiitaka kumsajili kiungo huyo wa Manchester City majira ya joto yajayo.**



"Heri ya siku ya kuzaliwa. Kwa vicheko zaidi, hadithi zaidi, na machweo zaidi ya jua pamoja. Ninakuabudu na kukukosa. PS: inabidi tufanye upya picha zetu rafiki," **Mke wa Lionel Messi, Antonela Roccuzzo, akimtakia heri ya siku ya kuzaliwa mke wa nyota wa zamani wa Barcelona, Luis Suarez na familia yake, huku tetezi zikizidi kuvuma kuwa Suarez anayeichezea Gremio, anatajwa kuwa mbioni kujiunga na Inter Miami anayoitumikia Messi.**



"Hilo ndilo neno - nadhani anaunganisha kila mtu. Ana akili sana. Nadhani anakimbia kwa njia zinazovutia watu zinazozalisha nafasi na chaguzi kwa watu. "Leo [juzi] alifanya hivyo vizuri kwa sababu ilikuwa ngumu sana na nafasi zilikuwa ndogo sana kushambulia. Alitupa vitisho vingi na uwezekano wa kuunganishwa na kutafuta nafasi kwa ajili yetu," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akieleza kufurahishwa na uwezo mkubwa wa mshambuliaji wake, Leandro Trossard, wakati wakishinda 3-1 juzi dhidi ya Burnley.**



MWANASOKA WAKIKE NA BIASHARA




# OPPA AJA NA 'OPPA BURGER' FETTY MAVAZI

**Na Saada Akida**

KAMA yalivyo maisha ya kazini kwa kila mfanyakazi, pia kwa upande wa mpira wa miguu, kuna maisha baada ya soka, na kila mchezaji hana budi kujipanga kwa maisha yake ya baadaye pindi atakapotundika daluga.

**Je, kwa upande wa wachezaji wa mpira wa miguu wanawake hali ikoje? Wanatumiaje umaarufu wao kibiashara au kukuza vipato vyao nje ya mchezo huo kwa maisha ya sasa na baadaye?**

Haya ikijulikana kwa sasa soka la wanawake ni kati ya michezo inayokua kwa kasi hapa nchini na kuvutia watazamaji wengi ambao tofauti na miaka ya nyuma, sasa hukubali kuutumia muda wao kufutilia ama kwa kwenda uwanjani au kupitia luninga, fursa ambayo wachezaji wanaweza kutumia kama sehemu ya kukuza vipato vyao.

Hii ni kutokana na wachezaji wengi wa kike kujulikana kwa ustadi wao mkubwa uwanjani na kuwa mfano mzuri kwa wanawake wengine nje ya soka.

Kwa sasa kadri soka la wanawake linavyozidi kushika kasi nchini, licha ya mshahara wanaopata wanasoka wa kike ambao huwezi kuulinganisha na ule wa wanaume, taratibu wameanza kujitangaza katika biashara zao au ujasiriamali wanaofanya kama sehemu ya kuwaingizia kipato zaidi.

Hayo yanadhihirishwa na aliyekuwa mshambuliaji wa Simba na sasa anacheza soka la kulipwa Klabu ya Besiktas ya Uturuki, Oppa Clement, ambaye mbali na soka anajishughurisha na biashara aliyoipa jina la 'OPPA BURGER' iliyopo maeneo ya Sinza Mori, Dar es Salaam.

Oppa anasema anauza vinywaji laini kama Juice ambayo inamsaidia sana katika kuongeza kipato chake mbali na mshahara ambao analipwa kupitia soka.

Anasema licha ya kuwapo mbali kuna watu amewaajiri kwenye biashara yake hiyo ambao kila siku anapata mrejesho kutoka kwao na faida inayopatikana kuingizwa benki.

Oppa anaongeza "licha ya kuwa nimeajiriwa kwenye soka, lakini hata mimi nimeweza kutoa ajira kwa vijana wenzangu kwa kusimamia biashara yangu hiyo na kunipa mrejesho jinsi inavyoenda pamoja na kwamba nipo mbali, nje ya nchi.







"Ni kweli umaarufu nilioupata katika soka unasaidia kukuza na kutangaza biashara yangu ikiwamo hata kuvutia mashabiki zangu kuniunga mkono."

Anasema mafaniko ya soka la wanawake kwa sasa ni makubwa ukilinganisha na miaka ya nyuma, na kwamba kwa sasa wachezaji wanalipwa mishahara mikubwa kwa wanasoka wa nje, lakini hata hiyo midogo kwa wale wanaocheza soka la ndani kama unaweza kutunza na kuweka malengo ya kufanya kitu unaweza kufanikiwa.

"Nimefanikiwa kwa hilo. Hakuna ugumu kwa kutumia jila lako kwenye biashara kwa sababu familia niliyoitengeneza katika soka wanafahamu kitu gani ninachokifanya nje ya uwanja, hali iliyonishawishi kufungua biashara yangu kwa kuipa jina langu la (OPPA BURGER) ," anasema Oppa.

Anasema anatambua mchango wa wanahabari na mitandao ya kijamii kwa sababu yote imefanikiwa kutengeneza jina lake hadi sasa katika soka pamoja na biashara yake.

"Kwangu mpira ni kazi wala si 'hobi', niko makini kwenye ofisi yangu ili nilipwe kipato kizuri ninachokipata kwani kinanisaidia. Sasa hivi soka la wanawake Tanzania linapiga hatua na wengi tumeanza kutoka kucheza soka la kulipwa nje," anasema nyota huyo na kuongeza:

"Usione wachezaji wa kike wanajituma uwanjani kwa dakika 90 au 120 pekee, bali juhudi na jitihada zao pia wanazifanya nje ya uwanja kwenye kutafuta kipato kingine ikiwamo biashara ambayo hutumia umaarufu wao waliopata kwenye soka."

Kuna ambao tayari wamefanikiwa, lakini baadhi ya wachezaji wengine ambao hawana biashara kupitia nyota huyo ambaye anabiashara, wameshawishika na kuwa kwenye mchakato wa kuanza kufungua biashara zao.

Martha John, ni miongoni mwa wachezaji ambao wanamiliki biashara, nyota huyo anayecheza kwenye kikosi cha Baobob Queens inayoshiriki Ligi ya Wanawake Tanzania Bara, anasema hana biashara yoyote lakini mikakati yake ni kumiliki mgahawa.

Anaongeza kuwa anaamini kuwa kufanya biashara ya mgahawa kwa kutumia jina lake ambalo amelitengeneza kupitia soka atafanikiwa malengo yake kimaisha.

"Kwa sasa niko katika mpira tu, lakini nina ndoto za kuwa mfanyabiashara wa mgahawa, ninaimani kupitia soka nitafanikisha mipango yangu. Ninaimani ya kazi yangu hii ya soka inaweza kuitangaza biashara yangu.

"Nimeona hapa kwenye klabu yetu wanauza zabibu na ubuyu, naona jinsi ambavyo wanawatumia wachezaji kutangaza biashara hizo, ninaimani hata nitakapoanzisha najua nitakapoanzia biashara yangu, na nitapata wateja kwa sababu ya jina langu kujulikana kwenye soka," anasema nyota huyo.

Wanasoka wengine wa kike akiwamo Fatma Issa. 'Fetty Densa,' mwenye biashara ya duka la nguo za kike, lakini pia amefanikiwa kutengeneza na kuuza T-shirt zenye jina lake (FETTY DENSA) na kununuliwa na jinsia zote mbili.

Huku akitumia mitandao ya kijamii na wachezaji wenzake au watu maarufu na wengine kutangaza jina lake kupitia biashara yake mbali na watu kumjua ndani ya uwanja.

## JE, WAJUA?



KWA mujibu wa mshambuliaji wa Manchester City, Phil Foden, beki wa pembeni mgumu zaidi kwake kuwahi kukabiliana naye ni nahodha wa Chelsea, Reece James.





# Muswada wapendekeza muda wadau kuwasilisha taarifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUSWADA wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi sura ya 278 kifungu cha 13 umependekeza kutenganisha muda wa mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kidini na asasi za kiraia kuwasilisha kwa msajili taarifa za gharama zilizotumika katika shughuli za uchaguzi.

Mapendekezo hayo yaliyowasilishwa bungeni na serikali mwishoni mwa wiki, marekebisho hayo yanalenga kupunguza muda wa kuwasilisha taarifa hizo, kipindi cha uchaguzi mdogo kwa kuwa kipindi hicho shughuli zinakuwa chache ikilinganishwa na kipindi cha uchaguzi mkuu.

Aidha, kifungu cha saba kinarekebishwa ili kuondoa takwa la wagombea kuwasilisha taarifa kuhusu timu ya kampeni kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Katibu Tawala wa Wilaya na Ofisa Mtendaji Kata na badala yake ziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Lengo la marekebisho hayo ni kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinawasilishwa kwa watu sahihi kwa kuwa sio mara zote Mkurugenzi wa Halmshauri na Katibu Tawala wa Wilaya wanakuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Kadhalika, kifungu cha tisa kinarekebishwa kwa kuboresha utaratibu wa kuchukua na kuwasilisha fomu za tamko la gharama za uchaguzi, ili fomu hizo zichukuliwe kwa msimamizi wa uchaguzi wakati mtia nia anachukua fomu za kuomba uteuzi na kuwasilishwa wakati wa kurejesha fomu za uteuzi.

Lengo la marekebisho hayo ni kutoa muda wa kutosha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kupitia taarifa zinazowasilishwa na watia nia kuhusu gharama wanazokusudia kutumia katika uchaguzi kabla hawajaanza shughuli za kampeni.

Pia, kifungu cha 18(2) kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha muda wa kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi wakati wa uchaguzi mdogo.

Lengo la marekebisho hayo ni kutenganisha muda wa kuwasilisha taarifa hizo wakati wa uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo kwa kuwa chama cha siasa hakiwezi kusubiri miezi sita ndipo kiwasilishe taarifa ya gharama za uchaguzi panapokuwa na uchaguzi mdogo.

Aidha, kifungu hicho kinarekebishwa pia ili kuondoa sharti la vyama vya siasa kuwasilisha stakabadhi halisi za matumizi ya gharama za uchaguzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, ili stakabadhi hizo zibaki kwenye vyama kwa ajili ya kuwasilishwa kwa mkaguzi.



Mkuu wa wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (aliyevaa kanzu) akikagua gwaride la Jeshi la akiba la mgambo waliohitimu mafunzo na kuhitimisha katika Kata ya Kizota Jiji la Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri Mavunde kukutana na watoa huduma sekta ya madini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde amesema atakutana na watoa huduma wote kwenye sekta ya madini, ili kuwasaidia wachimbaji wadogo na kuongeza idadi ya wafanyabiashara kwa lengo la kuchangia pato la taifa.

Mavunde aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa alipokuwa akifungua semina ya Jukwaa la Uzinduaji 2023 iliyoandaliwa na Taasisi ya HakiRasilimali.

"Natarajia kufanya hivyo kabla ya mwezi huu kuisha nahitaji kuona Watanzania wanakuwa na ushiriki mkubwa katika sekta ya madini,"alisema Mavunde.

Aidha, aliwataka wachimbaji madini na watoa huduma kwenye sekta hiyo, ili kuhakikisha wanasaidia kupiga hatua katika biashara wanazofanya.

Waziri Mavunde aliwataka wadau kwenye sekta ya madini kuacha kuoneana wivu kwenye biashara hiyo, badala yake aliyeko juu amvute na wa chini ili shughuli zao ziwe na tija kwa taifa.

Waziri Mavunde aliwapongeza aasisi hiyo kwa kuandaa jukwaa hilo ambalo linasaidia kushawishi jamii kuingia kwenye biashara ya madini.

Mkurugenzi wa Taasisi ya HakiRasilimali, Adam Antony alisema wameandaa Jukwaa hilo ili kuhakikisha wadau wanapata nafasi ya kutoa kero zao kwa ajili ya kufanyiwa kazi na serikali.

Alisema katika jukwaa hilo la uziduaji wadau wametoa maoni mbalimbali ambayo wao kama waandaaji wa jukwaa hilo wanaamini zitafanyiwa kazi ili sekta hiyo izidi kupiga hatua.

Antony alifafanua zaidi kuwa katika kongamano hilo, wadau wamejadili mazingira rafiki ya uwekezaji, haki za binadamu, uwazi wa mikataba ikiwemo utoaji leseni na ushiriki wa wanawake katika sekta ya madini.

# Rais Samia kuongoza ujumbe utakaohudhuria COP28 Dubai

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuongoza ujumbe wa Tanzania kushiriki Mkutano wa 28 wa nchi wanachama wa mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi (COP28) unaotarajiwa kufanyika Dubai.

Mkutano huo utasaidia Tanzania kuandaa na kutekeleza miradi ya kukabiliana na majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, kujenga uwezo wa nchi kuhusu masuala ya hifadhi ya mazingira na kuongeza wigo kwa nchi katika kupata fursa za mafunzo na ajira kwa vijana katika ngazi za kimataifa.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, alisema mkutano huo unalenga kuongeza chachu ya uwekezaji wa kimataifa kwa kutumia fursa katika sekta kwa kuvutia wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali duniani kote, ili kufahamu fursa za uwekezaji zilizopo na zinazopatikana katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waziri huyo alisema pamoja na mkutano mkuu wa COP28, kutakuwa na mikutano mingine ya awali inayohusisha viongozi na wataalamu ambayo huandaliwa na nchi au taasisi husika.

Alisema katika mikutano hiyo Rais Samia atakutana na viongozi mbalimbali na wakuu wa Nchi na Mashirika ya Kimataifa na lengo ni kusaidia nchi katika utekelezaji wa miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kujenga uwezo wa nchi kuhusu masuala ya hifadhi ya mazingira kwenye sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi, uchumi wa buluu, nishati, na udhibiti wa taka za plastiki.

"Pia kuiwezesha nchi kupata fursa ya nafasi za vijana katika mafunzo kwa vitendo (internship) kwenye Sekretarieti ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi na fursa za upatikanaji wa ajira kwa vijana.

"Kusaidia nchi yetu kupata, kuandaa na kutekeleza miradi ya kukabiliana na majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, kujenga uwezo wa nchi kuhusu masuala ya hifadhi ya mazingira na kuongeza wigo kwa nchi katika kupata fursa za mafunzo na ajira kwa vijana katika ngazi za kimataifa.

## Spika Tulia: Wakataeni wanaohamasisha vurugu

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

WANANCHI jijini Mbeya wametakiwa kuwakataa wanasiasa na wanaharakati wanaohamasisha vurugu na kulifanya jiji hilo kuwa kitovu cha fujo kwa maelezo kuwa ni hali inayoweza kukwamisha shughuli za maendeleo.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliyasema hayo juzi alipokuwa anahutubia mamia ya wananchi waliojitokeza katika Uwanja wa Ruanda Nzovwe kwa ajili ya kumpokea kwa mara ya kwanza tangu alipochaguliwa kuwa Rais wa Mabunge duniani (IPU).

Alisema kitendo cha yeye kuaminiwa na kuchaguliwa kushika nafasi hiyo kubwa kimataifa, kinalifanya jimbo la Mbeya Mjini kuheshimika, hivyo ili kuendelea kutunza heshima hiyo ni lazima waepuke vurugu zisizokuwa na maana.

"Kama ambavyo rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan alivyotuheshimu, kama ambavyo wabunge wote wa nchi hii walituheshimu na kama ambavyo dunia nzima imetuheshimu, basi na sisi tulinde heshima hii kwa kuwakataa wanaohamasisha fujo," alisema Dk. Tulia.

Alisema tangu alipochaguliwa kuwa mbunge wa Jimbo hilo amekuwa akihamasisha shughuli mbalimbali za maendeleo na kutekeleza ahadi mbalimbali alizoahidi.

Kwa mujibu wa Dk. Tulia, barabara ya njia nne ambayo imeanza kujengwa, miradi na maji, afya na elimu ambayo inatekelezwa ndani ya jiji hilo inatokana na hamasa na ushawishi wake serikalini.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema hivi karibuni kuna baadhi ya watu waliibuka wakawa wanawatukana viongozi mbalimbali wa serikali akiwemo Dk. Tulia hali ambayo ilikuwa inaashiria kuwashushia heshima viongozi hao.

Alisema baadhi ya watu hao walikuwa wanatukana matusi wakiwa kwenye nyumba za ibada jambo ambalo lilikuwa ni baya zaidi na kwamba wengine tayari wameshachukuliwa hatua.

"Tutahakikisha hali ya ulinzi na usalama ndani ya jiji hili inakuwa nzuri, ili ili uweze kutekeleza majukumu yako kwa amani na utulivu, mimi ndiye mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huu kwahiyo nikuhakikishie kwamba tutakulinda," alisema Homera.

Kwa upande wake Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela alisema chama hicho kitahakikisha kinamlinda Dk. Tulia katika kipindi chote atakachokuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini.

# H'shauri yahamasisha ulaji vyakula asili kukabili udumavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya kwa kushirikiana na wadau wa lishe nchini, imeanza kuhamasisha wananchi kula vyakula vya asili, ili kukabiliana na matatizo mbalimbali ya lishe ikiwemo udumavu kwa watoto.

Mamlaka hiyo mwishoni mwa wiki ilifanya tamasha maalumu la kuhamasisha wananchi kutumia vyakula bora, katika mradi wa msosi asilia ambapo viliandaliwa vyakula mbalimbali vya asili na wataalamu wa lishe wakatoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya vyakula hivyo.

Mradi huo wa msosi asilia ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya uongezaji wa thamani wa Kahawa, Chai na mazao ya bustani ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kutekelezwa katika mikoa mbalimbali nchini.

Ofisa Lishe wa Jiji la Mbeya, Itika Mlagalila alisema kutokana na miongozo ya lishe ambayo imekuwa ikitolewa na Wizara ya Afya, wamekuwa wakihamasisha zaidi uboreshaji wa lishe kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Alisema kupitia mradi wa msosi asilia, wanashirikisha makundi yote ya kijamii wakiwemo watu wazima, ili waepuke matumizi ya vyakula vya kisasa na badala yake wawe wanatumia vyakula vya asili ambavyo upatikanaji wake ni rahisi.

Alisema vyakula hivyo ni vizuri kutokana na kupatikana kirahisi na kuwa na virutubisho vingi ambavyo ni muhimu kwa afya ya binadamu wa rika zote.

"Wote tunafahamu ukiwa na afya njema utafanya kazi vizuri na serikali itanufaika na nguvu kazi yako, lakini hiki tunachofanya hapa leo lengo ni kuwa na jamii yenye afya bora, kwahiyo sisi kama serikali tunawashukuru wadau wetu ambao mmeanzisha mradi huu, tutaendelea kushirikiana nanyi wakati wote na tunaamini matamasha ya aina hii yanaweza yakaendelea kujirudia," alisema Itika.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mradi wa Agri-Thamani, Neema Lugangira, Mratibu wa wadau wa mradi huo, Famba Kazimoto alisema mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano na wizara ya Kilimo pamoja na Shirika la Chakula Duniani (FAO).

Alisema lengo la kufanya matamasha ya vyakula vya asili ni kuwahamasisha wananchi kurejea kwenye asili kwa kula vyakula vilivyokuwa vinaliwa na wazee wa zamani ambavyo vilikuwa vinawafanya wawe na afya njema.

Alisema kutokana na mabadiliko ya tabia za wananchi, ikiwemo ulaji wa vyakula usiokuwa sahihi yapo baadhi ya magonjwa ambayo yameanza kuibuka na kusumbua jamii hasa yale ambayo siyo ya kuambukizwa.

"Tunachojaribu kufanya hapa ni kuwakumbusha Watanzania kwamba usasa usiwafanye wasahau tulikotoka, lakini pia tunawakumbusha Watanzania kwamba usasa una madhara kama haya magonjwa," alisema Kazimoto.

Ofisa Lishe wa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Cecilia Mtega alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa nchini inayoongoza kwa uzalishaji wa aina mbalimbali za mazao ya vyakula.

Alisema pamoja na uwepo wa vyakula hivyo bado mkoa huo umekuwa ukikabiliwa na tatizo la udumavu kwa watoto hali ambayo inasababishwa na mifumo ya ulaji.

Alisema kwa sasa tatizo hilo la udumavu limeanza kupungua baada ya serikali kuanzisha mikakati mbalimbali ya kupambana na tatizo hilo na hivyo akasisitiza kwamba tamasha hilo la msosi asilia linasaidia pia kuimarisha mapambano hayo.



Katibu Tawala Mkoa wa Songwe, Happiness Seneda akimchachamalia mkandarasi wa kampuni ya Janta Construction Co Limited kwa kukwamisha mradi wa maji wa Msangano -Naming'ong'o akimtaka akatoe maelezo kwa Mkuu wa mkoa kabla ya kunyang'anywa kandarasi hiyo. **PICHA: YASIN IBRAHIM**

# RC Njombe aonya udanganyifu, uchakachuaji mbolea nchini

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewataka wafanyakazi wa makampuni na wazalishaji wa mbolea nchini, kuepuka udanganyifu na uchakachuaji wa mbolea hali inayoumiza wakulima na kutia hasara taifa.

Mtaka aliyasema hayo mara baada ya kuzindua ghala la kuhifadhia mbolea za kampuni ya ITRACOM ya mkoani hapa.

Alisema msimu wa kilimo uliokwisha ulifanyika udanganyifu na uchakachuaji wa mbolea jambo ambalo siyo sawa.

"Kampuni moja sitaki kuitaja jina kwa sababu ya biashara hapa Njombe, msimamizi wa ghala alifanya mchezo kwenye kupaki mbolea aina hiyo anaweka mchanga,mteja anajua ni mbolea imefungwa kumbe ni mchanga lakini tulipata wasimamizi wa magodauni wanafanya michezo na wafanyabiashara ambao sio waaminifu," alifafanua Mtaka.

"Mfuko umepimwa kilo 25 unapunguzwa kilo nne inabaki 21, mfuko ni kilo 50 anatoa tano inabaki 45, anachukua mchanga mweupe, anasaga chumvi anachanganya hadi mchele kwenye mbolea," alibainisha.

Mkuu huyo wa mkoa alitoa wito kwa wasimamizi wa maghala kuwa waaminifu na kuacha michezo michafu, kwa sababu ya kuwaaminisha mabosi kwa kuchukua mchanga na kuweka kwenye maghala ili kuonekana kwamba mbolea ipo nyingi.

Hata hivyo, Mtaka aliongeza kuwa kwa msimu huu wa kilimo mahitaji ya mbolea kwa mkoa wa Njombe ni tani 112,000 na kutoa wito kwa wafanyabiashara kuchangamkia fursa ya kuwekeza ili wakulima wasikose mbolea.

Alisema ipo haja kwa wakulima mkoani Njombe kuwa na uelewa mkubwa wa mbolea hiyo inayozalishwa hapa nchini kwa kutumia malighafi za ndani, ikiwemo samadi ya ng'ombe ambayo hufanya ardhi kukaa na rutuba kwa muda mrefu na hivyo kupunguza matumizi ya mbolea mbadala kwa kiwango.

Mawakala wadogo wa pembejeo mkoa wa Njombe akiwemo Oraph Mhema waliomba serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza bei ya mbolea inayozalishwa na kusambazwa nchini.

"Mbolea za Intracom bado zipo bei kubwa sana,wanazalisha kilo 25 hawana kilo 50, lakini bado inagharama kubwa sana kwa hiyo haiwezi kushindana na mbolea za nje,kiwanda ni cha kwetu kama wanakwama kwenye uzalishaji serikali muingilie kati," alisema Mhema.

Mkurugenzi wa Biashara na Masoko Itracom Dk. Keneth Masuki alisema mbolea hiyo tayari imeshasambazwa zaidi ya mikoa 18 ambapo kwa msimu uliopita mbolea aina tatu zimezalishwa zikiwemo fomi otesha, fomi kuzia na fomi nenepesha.

"Mkakati wa usambazaji wa mbolea zetu kwa msimu uliopita tulifika mikoa karibu 18, sasa hivi tumeona tufungue maghala baadhi ili mbolea iwe karibu na wateja wadogo wadogo,mawakala ambao hawawezi kuchukua lori zima," alisema Masuki.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Njombe, Erasto Mpete aliitaka kampuni hiyo kuhakikisha inakuwa na mashamba darasa kwenye kata zote ili kuonesha ufanisi wa mbolea hiyo kwa wakulima.



## Maryam Mwinyi ataka jamii kuwa na hofu ya Mungu

**Na Mwandishi Wetu**

MKE wa Rais wa Zanzibar Mama Maryam Mwinyi, amesema ni wajibu kwa waumini kuombeana dua ili kupata jamii yenye hofu na Mwenyezi Mungu.

Aliyasema hayo jana baada ya dua maalum ya wanawake ya kumuombea Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi iliyofanyika Kikwajuni.

Alisema dua ni miongoni mwa ibada kubwa kwa mujibu wa vitabu vya dini na kuupongeza umoja huo wa wanawake kwa uamuzi huo.

"Niombeni nitakupeni hakika wale watakaofanya kiburi katika ibada yangu wakaacha kuniomba basi nitawaangamiza motoni," alinukuu maandiko ya kitabu cha dini na kusema kuwa waumini wana wajibu huo wa kumuomba Mwenyezi Mungu ili aendelee kuwaongezea neema, mapenzi na baraka.

Alisema ni jambo jema kuona wanawake kwa pamoja wamekusanyika kumuombea dua Rais kwa madhumuni ya kumtakia mema na mafanikio ambayo ni kielelezo cha mapenzi waliyonayo kwake na serikali anayoingoza kwa mafanikio yanaendelea kupatikana katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake.

Alisema kitendo hicho ni cha kizalendo na uungwana na ndio asili ya mwanamke mwema kufanya mambo ya kheri hasa ikizingatiwa mwanamke ni kioo cha familia na jamii nzima.

Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana kwa miaka mitatu ya uongozi wa Dk. Mwinyi, alisema hali hiyo inatokana na wananchi kuwa watulivu, wamoja, wenye amani, na mshikamano na hakuna nchi inayoendelea bila kuwa na misingi hiyo muhimu.

Alisema ni lazima kuzilinda tunu hizo ili serikali itekeleze malengo yake ya kuwaletea maendeleo na kuiwezesha nchi kupiga hatua za kimaendeleo kama inavyotarajiwa.

Aliwataka wanawake kuendeleza umakini katika kusimamia malezi ya watoto na kuwaombea dua ili kuwaongoa kuwa vijana wema.

Naye Mkuu ya Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja, Hamida Mussa Khamis, alisema Rais Mwinyi amejenga hospitali kila wilaya na moja ya mkoa ambao watumiaji wakubwa ni wanawake na watoto na hata katika sekta nyengine ikiwamo elimu na miundombinu ya maji.

Akisoma risala kutoka kwa wanawake hao, Amina Salum Khalfan, kutoka Jumuiya ya Abrar, alisema wameamua kukusanyika pamoja kwa lengo la kumuombea dua ya fanaka na mafanikio Rais wao na kiongozi wa nchi ili kuendelea kumpa mambo ya kheri.

Alisema Zanzibar imepata Rais mtulivu, mwaminifu na mpenda amani, umoja na mshikamano na kumzidishia kheri katika maisha yake yote ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Akitoa neno la Shukran Ukti Thania Mahomud, alisema wanawake wataendelea kumwombea dua Rais Mwinyi ili aendelee kufanya maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule, hospitali masoko, barabara na miundombinu mingine muhimu kwa jamii.

"Sisi wanawake tupo pamoja na kiongozi wetu usiku na mchana kuendelea kumuunga mkono katika kila hatua ya uongozi wake na tutaendelea kumuombea dua ili Mwenyezimungu aendelee kumpa afya na siha njema aendelee kututumikia vyema," alisema.

# Tanzania yajivunia usalama, amani kuvutia wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

USALAMA na amani nchini vimetajwa kuwa ni moja ya fursa muhimu ya kuitangaza nchi katika kukuza uwekezaji huku Tanzania ikijivunia tunu hizo.

Akizungumza baada ya ziara ya kutembelea maeneo ya uwekezaji visiwani Zanzibar wakiwa na wenyeji wao Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Binilith Mahenge, alisema pia Tanzania inajivunia uongozi bora wenye siasa safi chini ya Rais Samia ambaye amejipambanua kuifungua nchi.

Alisema juhudi hizo za Rais Samia zimesaidia kuweka taratibu mbalimbali za kufanya marekebisho ya mifumo ya uongozi ikiwamo sera na sheria, pia Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepambana na kuweka uwazi ili kukuza uwekezaji.

Alisema ZIPA na TIC zimepewa jukumu la kuvutia wawekezaji nchini na kuandaa mikakati ya wawekezaji kuingia nchini.

Alisema suala la uwekezaji ni ushindani kati ya Afrika Mashariki, Kusini mwa Afrika na dunia nzima na kwamba ni lazima kuwa na mikakati ya kuwaleta wawekezaji bila ya kuwa na changamoto.

"Tanzania pia ina sifa ya uwapo wa fursa nyingi za uwekezaji, vyombo vinavyosimamia uwekezaji ambavyo ni TIC na ZIPA, lakini haitoshi kwa sababu yapo maandalizi ambayo tunatakiwa tuyafanye ili kupata wawekezaji watakaofaidika na hizo fursa," alisema. Alisema mwekezaji anapokuja nchini analeta mtaji, teknolojia, ajira, utaalamu, ubunifu, huongeza uzalishaji na pato la taifa litaongezeka.

"Kazi yetu sisi kuona hatupotezi fursa za kupata wawekezaji na ndio maana tumekuja Zanzibar kwa wezetu ZIPA kujifunza, unapokuwa na mkakati kama walivyofanya wezetu tumetembelea bandari mbili, bandari jumuishi Mangapwani na bandari ya mizigo Fumba," alisema.

Aidha alisema hatua hiyo itasaidia mizigo kutokaa muda mrefu bandarini hasa ikizingatiwa kuwa wawekezaji huagiza vifaa vyao nje ya nchi na uwapo wa bandari hiyo ya mizigo utaondoa changamoto ya mizigo kutokaa muda mrefu bandarini.

Alisema ziara hiyo wamejifunza mambo mengi na uwekezaji huo ni mkubwa na unasaidia katika uwekezaji wa sekta nyingine na kuipongeza ZIPA kwa hatua hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa ZIPA, Sharif Ali Sharif, alisema wamefurahia ushirikiano kati yao na TIC na ziara imewapa faraja kufika Tanzania Bara kujifunza vitu mbalimbali walivyofanya.

Alisema ZIPA itaendelea kufuata sera na sheria ikiwamo ya maeneo huru kuyatangaza na kupata wawekezaji wakubwa na kuinua nchi kufikia maendeleo yanayotakiwa kufikiwa.

Peter Mjomba, Mkuu wa Operesheni wa Bandari ya mizigo Fumba, alisema imeanza kazi rasmi ya kushusha na kupakia mizigo kwa meli zinazotoka nje nchi mwanzoni mwa Oktoba mwaka huu na wameshapokea meli tatu za mizigo.

Alisema bandari hiyo ina uwezo wa kuhifadhi kontena za mizigo 3,600 na hushusha kontena 11 kwa muda wa saa moja.

Bodi ya wakurugenzi ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), ilitembelea Bandari jumuishi iliyopo ya Mangapwani Mkoa wa Kaskazini Unguja, uzalishaji wa vifaranga Maruhubi Mjini Unguja na Bandari ya mizigo iliyopo Fumba nje ya mji wa Zanzibar.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko akiwaongoza watendaji wakuu wa TAQA Arabia, JCG na TAQA Dalbit kukata utepe wakati wa uzinduzi wa kituo cha kwanza cha kujaza mafuta cha CNG na kituo cha ubadilishaji umeme nchini Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ZRCP kushirikiana na Wakala wa Serikali kidijitali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Kituo cha Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii Zanzibar (ZRCP), imetiliana saini mkataba wa ushirikiano na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (E-Government), kuhusu mabadiliko ya kiuchumi na kijamii ili kuipeleka nchi katika mtindo wa kidijitali.

Akizungumza jana baada ya hafla hiyo ya utiaji saini iliyofanyika juzi visiwani humo, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Juma Reli, alieleza maeneo mahususi watakayoshirikiana katika kutoa utaalamu wa mambo ya dijitali na kutayarisha hati zitakazosaidia kufanya malipo ya kimtandao.

Alisema taasisi yake inafanya kazi ya kupitia sera kwa kutumia utafiti na kuishauri serikali namna bora ya kuzimarisha na kufanya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii kweye mifumo mipya ya kidijitali kutoka utaratibu uliokuwa ukitumika zamani.

Alisema mfumo wa kisasa wa kidijitali sio rahisi kughushiwa kwa sababu unaundwa katika vituo mbalimbali na kama ukiharibiwa sehemu moja ni rahisi kujulikana.

Alisema ushirikiano huo na serikali utaleta ufanisi na kuiweka sawa mifumo yote ili kusomana na kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato.

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri wa Uchumi wa Kidijitali wa ZRCP, Nicholas Haan, aliishukuru Serikali ya Zanzibar kuiamini taasisi yao na kuahidi kufanya kazi ili kukidhi matarajio ya umma.

Seif Said, Mkurugenzi wa wakala wa serikali mtandao, alisema katika kuleta mabadiliko ya kidijitali ushirikiano wa taasisi binafsi na wananchi unahitajika ili kuhakikisha malengo yanafikiwa.

Alisema RRCP ina uwezo mkubwa katika masuala ya utafiti, kutoa taaluma na kuwaleta washirika wa maendeleo wenye uwezo wa kuchagia maarifa na rasilimali zinazohitajika kuimarisha mifumo kutochezewa.

Aidha, alisema taasisi hiyo itafanya utafiti ili kuhakikisha Zanzibar inapata uwezo wa kutumia teknolojia katika kufikia ustawi wa kiuchumi na kijamii kwa wananchi wake.

# AGRA yawajengea wanahabari uwezo uandishi wa mbegu bora



Wahariri wa vyombo mbalimbali kwenye picha ya pamoja, Bagomoyo, mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Mwandishi Wetu,** BAGAMOYO

VYOMBO vya habari nchini vimetakiwa kuandika habari zinazohusu maendeleo ya teknolojia ya mbegu ili kuchangia kilimo cha kisasa na kuwezesha usalama wa chakula na uimara wa uchumi katika kukabiliana na ongezeko la idadi ya watu na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Wito huo umetolewa katika kongamano la shirika linalojihusisha na kuendeleza mifumo ya chakula barani Afrika (AGRA) kwa waandishi wa habari lililofanyika Bagamoyo, mkoani Pwani.

Kongamano hilo ni matokeo ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), kutaka waandishi wa habari na wahariri kuandaliwa kikao cha kuelimishana kuhusu teknolojia ya habari ili kuwa na nafasi ya kujifunza namna ya kusaidia wakulima wa Tanzania.

Waandishi walielimishwa ukweli kuhusu uwezo wa teknolojia ya mbegu zilizoboreshwa na mbegu mseto nchini.

"Vyombo vya habari vina jukumu muhimu katika kuunda maoni ya umma na kupeleka sera. Kwa kuwapatia wataalamu wa habari ukweli, tunawasaidia kutoa taarifa na elimu kwa jamii pana, hivyo kuchangia katika kufanikisha kupokelewa kwa mazoezi bora ya kilimo." Vianey Rweyendela, Mkurugenzi wa AGRA Tanzania, alibainisha.

AGRA Tanzania imechangia maendeleo ya aina mpya 44 za mbegu zilizoboreshwa za mahindi, muhogo, maharage na soya kwa kushirikiana na taasisi za utafiti za serikali na washirika wa sekta binafsi. Aina 30 miongoni mwa hizo zimeingia sokoni.

Vilevile, AGRA imetoa mchango muhimu katika kuimarisha sekta ya mbegu kwa kutoa msaada kwenye thamani ya mnyororo wa mbegu, ikiwamo kujenga uwezo wa wazalishaji wa mbegu, kampuni za mbegu za ndani na wadau mbalimbali na kuchangia ukuaji na ustahimilivu wa sekta ya kilimo.

> Kuelewa teknolojia ya mbegu na uhusiano wake na mabadiliko ya tabianchi ni ufunguo wa uzalishaji wa mbegu endelevu na mustakabali wa kilimo chenye ustawi nchini Tanzania.

"Matumizi ya mbegu bora Tanzania kwa sasa ni asilimia 20 tu, hii inaonyesha kwamba ikiwa kiwango cha matumizi ya mbegu bora kitaongezeka, Tanzania itakuwa katika nafasi nzuri ya kufikia lengo lake la kuwa ghala kubwa la chakula barani Afrika," alisema Ipyana. Mwakasaka, Afisa wa Mpango wa Mbegu wa AGRA nchini.

Deodatus Balile, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania, aliipongeza AGRA kwa kujitolea kuongeza uwezo wa waandishi wa habari nchini katika sekta ya kilimo.

"Kuwa na weledi wa kina kuhusu mambo magumu ya kilimo ni muhimu kwa Tanzania inavyoazimia kuwa mzalishaji mkuu wa chakula barani Afrika," alisema. Alitilia mkazo umuhimu wa programu hizi za elimu, akishawishi kuongezeka kwa mara kwa mara ili kuhakikisha waandishi wa habari wanaweza kuchangia kwa ufanisi katika hadithi ya kilimo iliyoelimika vyema.

Alisisitiza zaidi umuhimu wa kimkakati wa maarifa haya: "Kuelewa wigo kamili wa masuala ya kilimo, kuanzia sayansi ya udongo na mbegu hadi sera, ni msingi kwa uandishi sahihi na unaweza kuweka Tanzania mstari wa mbele katika sekta ya chakula ya bara."

Mkufunzi katika warsha hiyo, Mtaalam wa uboreshaji wa mimea na mwanasayansi wa utafiti, Dk. Emmarold Mneney, alisema msimamo thabiti wa Tanzania kulisha Afrika, unahitaji kuwekeza zaidi katika uvumbuzi wa mbegu.

"Kuelewa teknolojia ya mbegu na uhusiano wake na mabadiliko ya tabianchi ni ufunguo wa uzalishaji wa mbegu endelevu na mustakabali wa kilimo chenye ustawi nchini Tanzania," alibainisha.

Amewataka wanahabari kuelewa mbegu, ufugaji, na uzalishaji wa madarasa tofauti ya mbegu, pamoja na uelewa wa mahitaji ya mbegu na utabiri wake.

Dk. Geradina Mzena, Mtaalam wa Uboreshaji wa Mimea (Plant Breeder) na mtaalamu mahususi wa jeni za molekuli (Molecular Geneticist), ambaye pia ni Meneja wa Kituo cha Taifa cha Rasilimali za Mimea za Kijenetiki katika TARI-HQ, alisisitiza umuhimu wa teknolojia ya uzalishaji wa mbegu kwa ajili ya kilimo cha mahindi:

"Mustakabali wa kilimo cha mahindi uko katika kutumia nguvu ya teknolojia ya uzalishaji wa mbegu za mseto na bora ili kuimarisha usalama wa chakula na uimara katika uso wa mabadiliko ya mandhari ya kilimo."

Dk. Mzena alisisitiza kwamba mseto, unaojulikana kwa uwezo wake wa mavuno makubwa, una changamoto moja. Mseto unahitaji mbegu mpya kila msimu.

Dk. Twalib Njohole, Msajili wa Haki za waboreshaji wa Mimea (Registrar of Plant Breeders Rights), alibainisha kwamba ili kulisha dunia, aina mpya, bora za mimea ni njia muhimu na endelevu ya kufikia usalama wa chakula katika muktadha wa ongezeko la idadi ya watu na mabadiliko ya tabianchi.

"Aina mpya zinaweza kuwa ufunguo wa kufikia masoko ya kimataifa na kuboresha biashara ya kimataifa kwa nchi zinazoendelea," anasema. Pia amesisitiza nafasi ya aina mpya za mimea katika kuboresha maisha katika maeneo ya vijijini na mijini na kukuza maendeleo ya kiuchumi.

Zera Mwankemwa, Afisa wa Uthibitisho wa Mbegu Taasisi ya Uthibitisho wa Mbegu Tanzania (TOSCI), anasema: "Uthibitisho ni muhimu ili kuhakikisha wakulima wanapata mbegu bora zenye uwezo mkubwa wa uzalishaji na zinazozingatia usalama wa mazingira." Mwankemwa anafafanua jukumu la TOSCI la kusimamia ubora wa mbegu zinazoingia na kutumika nchini ili zikidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

Anasisitiza kwa ushirikiano na wadau, TOSCI inaboresha mfumo wa uthibitisho kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa mbegu bora hasa kwa wakulima wadogo, ambao ni nguzo ya kilimo cha Tanzania. Jitihada hizo ni kwa ajili ya kuchangia mapinduzi ya kijani na kuongeza tija katika sekta ya kilimo, na hatimaye kuchangia kwenye ustawi na maendeleo endelevu ya taifa.

Pia, mfumo wa kisheria ambao TOSCI inafanya kazi; "Inasimamiwa na Sheria ya Mbegu Na. 18 ya 2003, kama ilivyorekebishwa mwaka 2017, pamoja na Kanuni za Mbegu za 2007, ambazo zilirekebishwa mwaka 2014. Mfumo huu wa kisheria unatupatia zana na mamlaka ya kusimamia sekta ya mbegu na kuhakikisha uadilifu na utendaji wake."

Kupitia michakato yake mikali ya udhibiti, TOSCI inachangia katika uzalishaji wa mbegu za ubora wa juu, ambazo kwa upande wake husaidia wakulima kufikia mavuno bora.

Baldwin Shuma, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Biashara ya Mbegu Tanzania (TASTA), anasisitiza uhusiano uliopo kati ya usalama wa chakula na usalama wa mbegu, akisema, "Usalama wa chakula unapaswa kupangwa sambamba na USALAMA WA MBEGU. Ni ushirikiano wa kimkakati kwa ajili ya mustakabali wa kilimo imara."

Anasisitiza umuhimu wa Tanzania kupunguza utegemezi wa mbegu zinazoagizwa kutoka nje, akibainisha, "Tanzania lazima ipunguze utegemezi wa mbegu zinazoagizwa. "Aliongeza msisitizo kuhusu umuhimu wa kujitosheleza katika uzalishaji wa mbegu ili kuhakikisha usalama wa chakula na uendelevu wa kilimo.

"Kuwezesha wazalishaji wa mbegu za ndani na kuongeza uwezo wao ni muhimu kwa kujenga sekta ya mbegu imara na endelevu," anasema.

Wawezeshaji wa mafunzo, wahariri wazoefu, Neville Meena na Jesse Kwayu kutoka Media Brains Tanzania, wamesisitiza umuhimu kwa tasnia ya habari kutofautisha kati ya "nafaka" (cereals) na "mbegu" (seeds). Utofautishaji huo unahakikisha utoaji taarifa sahihi na unachangia uelewa wa kina wa istilahi na mazoea ya kilimo.

"Kupitia mafunzo haya, tumetambua kwamba mbegu siyo bidhaa tu bali ni uhai kwa wakulima wetu na jiwe la msingi la maendeleo ya kilimo chetu," Absalom Kibanda, akisisitiza nafasi muhimu ya majadiliano yaliyoelimika na sahihi kuhusu maendeleo ya mbegu.

Apolinary Tairo, mwandishi nguli wa habari za utalii na kilimo, alisema kuwa amejifunza mambo ya thamani kubwa.

"Mafunzo haya yamepanua maarifa yangu kwa kiasi kikubwa. Sikuwa na ufahamu wa nafasi muhimu ambayo mbegu inacheza katika sekta yetu ya kilimo na juhudi kubwa zilizo katika kuhamasisha maendeleo yake. Ufahamu huu mpya bila shaka utaboresha ripoti zangu za kilimo siku za usoni. Kama mwandishi wa habari niliyejitolea, nimejizatiti kutoa taarifa zenye uelewa mpana na zenye kina kuhusu sekta ya kilimo.



Baadhi ya Wapalestina wakiondoka eneo la Kusini mwa ukingo wa Gaza, kwa kutumia barabarara kuu ya Salah al-Din, eneo la Bureij mjini Gaza, jana. **PICHA: AP**

# Hofu yatanda, mashambulizi Al Shifa

## • Watoto waliolazwa waondolewa

**Na Christina Mwakangale**

ISRAEL imeeleza sababu kadhaa za mashambulizi yaliyofanyika usiku wa kuamkia jana.

Katika hospitali ya Al Shifa, imeelezwa kwamba wamebaini kituo hicho cha huduma za afya ni sehemu ya eneo Kuu la kundi la Hamas.

Shirika la Afya Duniani (WHO), limesema limepoteza mawasiliano na hospitali hiyo, huku Israel ikisema itazingatia na kusaidia kuwahamisha watoto katika hospitali hiyo, BBC imesema.

Akizungumza jana kwenye televisheni ya BBC, Balozi mstaafu wa Ubalozi wa Marekani nchini Israel, David Friedman, amesema uchunguzi wa kiusalama umebaini hilo, uhusiano kati ya kundi la Hamas na eneo la hospitali hiyo.

Taarifa kutoka hospitali hiyo ikiwamo matabibu, wanasema kituo hicho pekee kilichosalia kutoa matibabu na kutegemewa na wengi, kinakosa umeme, chakula na maji huku kikizingirwa na vifaru.

Kadhalika, wanaeleza kupewa muda wa saa moja pekee, ili kuwahamisha wagonjwa wakiwamo watoto ambao baadhi walikuwa katika Idara ya Uangalizi Maalum (ICU).

Mashambulizi yanayofanywa na jeshi la Israel katika eneo la Gaza, yana takribani wiki tano, tangu Oktoba 7, mwaka huu, kundi la Hamas lilipotekeleza shambulio dhidi ya Israel, na wakiuawa Waisrael 1,400.

Aidha, Wizara ya Afya ya Palestina, imesema takribani Wapalestina 11,000 wameuawa katika mashambulizi hayo na kati yao wapatao 4,000 ni watoto na wengine ni wanawake na wazee.

> **“Hakuna mahali popote na hakuna mtu aliye salama” amesema, na kuongeza kuwa wahudumu wa afya wanajitahidi kujaribu kudhibiti mahitaji ya kiafya ya watu milioni 2.3.**

Kwa mujibu wa mwandishi wa BBC, mkakati wa jeshi la Israel umejikita katika awamu tatu. Awamu hii ya pili inalenga kuondoa upinzani kutoka kwa Hamas.

Awamu ya kwanza ilikuwa ni kuharibu miundombinu ya kundi hilo na ya tatu itakuwa kuiondoa Israel katika Ukanda wa Gaza na kuanzisha hatua mpya za usalama kwa raia wa Israel.

Juzi, pia iliripotiwa kuwa Hamas iko tayari kubadilishana mateka zaidi ya 220 inaowashikilia huko Gaza na wafungwa wa Kipalestina katika magereza ya Israel.

Katika maelezo yake, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu amesema suala hilo, kuhusu wafungwa lilijadiliwa na baraza la mawaziri la vita la Israel, lakini alikataa kutoa maelezo zaidi.

Netanyahu, amenukuliwa na vyombo vya kimataifa, akisema Israel haitaweka silaha chini huko Gaza.

Kumekuwa na maelefu ya maandamano mjini London nchini Uingereza, kutoa wito kusitishwa kwa mapigano huko Gaza. Pia, maelfu ya wakazi wameendelea kuhama Kaskazini mwa Gaza kuelekea Kusini, kwa kutumia njia maalumu za kupitia.

### UMOJA WA MATAIFA

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, mwishoni mwa wiki, limekutana tena kujadili mzozo unaoendelea wa Israel na Palestina huku mazungumzo yakiendelea, ili kufikia baadhi ya muafaka kuhusu vita inayoendelea Gaza, ndani ya chombo hicho chenye wajumbe 15.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Afya Duniani (WHO), Dk. Tedros Ghebreyesus, amesema baada ya kuishi katika vita akiwa mtoto na mzazi, anaelewa vyema mateso na hofu inayopatikana huko Gaza hii leo.

Amesema chombo hicho hakitumiki kwa madhumuni ambayo kilianzishwa na sio kwa karne ya 21.

Ili kibaki kuaminika, kuwa muhimu na nguvu ya kuleta amani katika dunia yetu, nchi wanachama lazima zichukulie kwa umuhimu suala la kulifanyia mageuzi Baraza la Usalama.”

### MSAADA WA HARAKA WAHITAJIKA

Mkuu huyo wa WHO amesema njia bora ya kuwaunga mkono ni kuwapa kile wahudumu wa afya wanachohitaji, ili kuokoa maisha.

Takriban tani 63 za msaada huo zimetumwa, lakini fursa ya kuingiza msaada huo isiyo na kikomo ikihitajika kuweza kuwafikia raia, ambao hawahusiki na mzozo huo.

Wastani wa malori 500 kwa siku yalivuka hadi Gaza na vifaa muhimu.

Tangu Oktoba 21, mwaka huu, ni malori 650 tu ya misaada ndio yameingia katika eneo hilo, amesema.

WHO imeendelea kutoa wito wa kusitishwa kwa mapigano. Pia ametoa wito kwa Hamas kuwaachilia mateka hao na kuitaka Israel kurejesha usambazaji wa maji, umeme na hasa mafuta.

Pia amezitaka pande zote mbili kuheshimu wajibu wao chini ya sheria za kimataifa za kibinadamu.

“Ninaelewa kile ambacho watoto wa Gaza lazima wanakipitia kwa sababu nilipokuwa mtoto, nilipitia vivyo hivyo” amesema, akikumbuka sauti za risasi za tracer, milio ya risasi na harufu na taswira ya vita.

“Najua nini maana ya vita. Watoto na familia za Israel na Palestina wanataka amani na usalama.”

Hali katika eneo la Gaza ni ya kusikitisha amesema mkuu huyo wa WHO, kuanzia kwenye hospitali zinazofanya operesheni bila ya ganzi hadi ukweli kwamba mtoto huuawa kila baada ya dakika kumi.

“Hakuna mahali popote na hakuna mtu aliye salama” amesema, na kuongeza kuwa wahudumu wa afya wanajitahidi kujaribu kudhibiti mahitaji ya kiafya ya watu milioni 2.3.

Amesema anasikitishwa sana na mateka ambao bado wanashikiliwa na atakutana na familia zaidi wiki ijayo mjini Geneva.

Amesema pia anaelewa hasira, huzuni na woga wa watu wa Gaza, wanaoteseka kuharibiwa kwa familia zao, nyumba zao, jamii zao na maisha wanayojua.

Israel na Palestina zote zimealikwa kushiriki katika mkutano huo, bila pingamizi.

***IMEANDALIWA KWA MSAADA WA VYOMBO VYA HABARI VYA KIMATAIFA***

## HABARI MICHEZO

# CHAMPIONSHIP SASA MWENDO WA KUVUTANA MASHATI KILELENI

Na Adam Fungamwango

NI mwendo wa kuvutana mashati na kushushana kileleni, hicho ndicho kinachoendelea kwenye Ligi ya Championship baada ya TMA ya Arusha nayo kuvutwa chini na Mbeya Kwanza ikirejea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo wiki hii baada ya mechi za raundi ya kumi kupigwa.

**TMA iliongoza wiki nzima iliyopita ikiwa imeiengua KenGold ya Mbeya, ambayo nayo ilikuwa imeipiku Mbeya Kwanza.**

Ushindi wa bao 1-0 ilioupata dhidi ya Stand United juzi umeirudisha Mbeya Kwanza kileleni, baada ya wiki tatu.

Lilikuwa ni bao pekee lililofungwa dakika ya 70 na Ramadhani Kapera kwenye Uwanja wa Mwadui Complex, Shinyanga ambalo limewarudisha kileleni kwa kujikusanyia pointi 23.

TMA ilikuwa inaongoza tangu wiki iliyopita hadi juzi, ilipolazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania, mechi ikipigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, matokeo ambao yameifanya kushuka hadi nafasi ya pili ya msimamo ikiwa na piinti 22 kwa mechi 10 ilizocheza.

KenGold ambayo iliongoza ligi hiyo, wiki mbili zilizopita, ipo nafasi ya tatu ya msimamo ikiwa na pointi 20, ikiwa na mechi moja mkononi, ikitarajiwa kucheza dhidi ya Copco ya Mwanza na kama itashinda, itafikisha pointi 23 kama Mbeya Kwanza na kuongoza ligi au kutoongoza kutatokana na idadi ya mabao ya kufunga kwa timu zote.

Matokeo ya mechi nyingine ya Ligi ya Championship, kusaka timu mbili zitakazopanda Ligi Kuu msimu ujao moja kwa moja na nyingi kucheza mechi ya mchujo, yalikuwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, wakati Comsopolitan ilipotoka sare ya bao 1-1 Green Warriors, huku Biashara United ikijipigia kibonde kwenye ligi hiyo, Ruvu Shooting mabao 3-0, kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.






Wanafunzi wa Shule ya Msingi Hazina ya Magomeni jijini Dar es Salaam wakionyesha vipaji vyao wakati wa mahafali ya shule hiyo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki shuleni hapo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Shule ya Hazina yaanza kulea vipaji*

Na Joseph Mwendapole

SHULE ya Msingi Hazina ya Magomeni, Dar es Salaam, imeanza kulea vipaji vya wanafunzi katika sanaa mbalimbali kama vile mitindo, kuimba, sarakasi na mpira wa miguu.

Shule hiyo imesema wanafunzi wa shuleni hapo wameonesha kuwa na vipaji kwenye maeneo mbalimbali na ndiyo sababu ikavutiwa kuanza kuibua vipaji hivyo na kuviendeleza.

Akizungumza kwenye mahafali ya shule hiyo mwishoni mwa wiki, Mkuu wa shule hiyo, Omari Juma, alisema shule hiyo imekuwa na programu ya michezo kwa ajili ya kuangalia vipaji mbalimbali vya wanafunzi.

Alisema michezo mbali na kuimarisha afya za wanafunzi, lakini inaweza kusaidia kwa wale wenye vipaji kuwa chanzo cha mapato kama baadhi ya wasanii na wachezaji wa michezo mbalimbali waliofanikiwa.

Alisema mbali na kuendelea kuongoza kitaaluma, Hazina itaendelea kuibua na kulea vipaji vya wanafunzi ili viweze kuwasaidia kwenye maisha yao ya kila siku kwani upo ushahidi wa watu waliofanikiwa kutokana na vipaji vyao.

"Kuna mwanafunzi mwingine anaweza kuwa wa kawaida darasani, lakini akawa na kipaji kikubwa sana ambacho akikiendelezwa anakuja kuwa msanii mkubwa sana na anaingiza fedha nyingi kwa hiyo utaratibu wa kuibua vipaji uwe endelevu kwa shule nyingi," alisema Omari

Mmoja wa wazazi wa waliohudhuria mahafali hayo, Asha Aboubakary, aliipongeza shule hiyo kwa kuendesha program ya kuibua vipaji vya wanafunzi kwani wamejionea wenyewe namna wanafunzi walivyoonyesha umahiri kwenye sanaa.

"Kwa kweli tumeona wenyewe umahiri wa wanafunzi wa Hazina kwenye sanaa na mitindo mbalimbali kuanzia sarakasi, mitindo ya mavazi, kuimba na kucheza kwa hiyo vipaji huwa vinalelewa tumeona vipaji vingi kwa hiyo wavilee vinaweza kuja kuwasiaida hawa watoto," alisema

# KVZ sasa yakiri Ligi Z'bar ngumu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kukaliwa tena kooni katika mbio za Ligi Kuu Zanzibar kwa kulazimishwa sare ya bao 1-1 juzi dhidi ya Walinzi wa Mipaka, Uhamiaji FC, hatimaye sasa Maafande wa KVZ wamekiri kuwa matokeo hayo yanatokana na ligi hiyo kuwa ngumu.

Mchezo huo uliochezwa juzi katika Uwanja wa Mau B, ulivuta hisia kubwa ya mashabiki wa kila timu waliofika uwanjani hapo.

Kwa matokeo hayo KVZ SC imefikisha alama 20 ikiwa nafasi ya pili huku vinara wa ligi hiyo, JKU SC wakiwa na alama zao 23 katika michezo 10 waliyocheza.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Kocha Mkuu wa timu ya KVZ, Ali Mohmed, alianza kwa kukiri kuwa michezo yote hivi sasa inazidi kuwa migumu licha ya wachezaji kujituma na kucheza kwa kutaka matokeo.

Alisema mchezo huo tangu hapo awali alijua anaenda kucheza na timu yenye uwezo mkubwa na yenye kiu ya kusaka matokeo na yeye alijiandaa kukabiliana na hali hiyo licha ya matokeo kuwa sare.

Alisema wachezaji wake walicheza vizuri katika dakika zote za mchezo licha ya mapungufu kadhaa yaliyojitokeza ya kukosa magoli mengi ya wazi yaliyotokana na presha ya mchezo wenyewe.

"Michezo yote katika kuelekea mwishoni mwa mzunguko huu wa kwanza ni migumu sana, kila timu inapambana kuhakikisha inapata matokeo mazuri, hivyo lazima tuwe na mikakati imara ili kupata matokeo mazuri," alisema.

Aidha, alisema kupata matokeo mbaya katika michezo mitatu haijavunja mipango ya mbio za ubingwa wa ligi hiyo, bali ndiko kumewapa nguvu na matumaini makubwa ya kupambana.

Hata hivyo, alisema wanajipanga kuhakikisha mchezo wao wa 11 watakaocheza Ijumaa wiki hii dhidi ya Maafande wa Zimamoto SC wanapata alama tatu.

**Michezo yote katika kuelekea mwishoni mwa mzunguko huu wa kwanza ni migumu sana, kila timu inapambana kuhakikisha inapata matokeo mazuri, hivyo lazima tuwe na mikakati imara ili kupata matokeo mazuri.**

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS AITAKA CITY

KIUNGO wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27, anapendekeza kuhamia Newcastle United kwa mkopo Januari badala ya Juventus. ***(Calciomercato)***

### BRANDT AWINDWA ARSENAL

KIUNGO mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Ujerumani, Julian Brandt mwenye umri wa miaka 27, anawindwa na Klabu za England, Arsenal na Newcastle United. ***(Mirror)***

### SANTOS NA MUSTAKABALI

CHELSEA inapanga mazungumzo na Nottingham Forest ili kutatua mustakabali wa kiungo wa kati Mbrazil Andrey Santos mwenye umri wa miaka 19, ambaye yuko kwa mkopo katika kikosi cha Steve Cooper, lakini amecheza mara moja pekee kwenye Ligi Kuu msimu huu. ***(Mirror)***

### AYEW AJIUNGA HAVRE

MSHAMBULIAJI wa Ghana, Andre Ayew mwenye umri wa miaka 33, amejiunga na Le Havre baada ya kuondoka Nottingham Forest mwishoni mwa msimu uliopita. ***(Fabrizio Romano)***

### LUIZ ALENGWA ARSENAL

ARSENAL imemfanya kiungo wa kati wa Aston Villa na Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 25, kuwa mshezaji namba moja wanayelenga kumnunua Januari. ***(Mirror)***

### LAPOTEGUI AWANIWA SAUDIA

KLABU ya Saudi Srabia ya Al-Ittihad iko kwenye mazungumzo ya juu na Mhispania mwenye umri wa miaka 57 na kocha wa zamani wa Wolves na Real Madrid, Julen Lopetegui. ***(Ben Jacobs)***

### PARTEY KUBAKI EMIRATES

ARSNENAL walitaka kumtoa kiungo wa kati wa Ghana, Thomas Partey mwenye umri wa miaka 30, lakini jeraha lake la paja lina maana kwamba anaweza kuendelea kubakia katika klabu hiyo baada ya kipindi cha majira ya baridi kali. ***(Football Insider)***

### ROMEU KUNG'OLEWA BARCA

GIRONA inataka kumsajili tena kiungo wa kati wa Hispania, Oriol Romeu mwenye umri wa miaka 32 kutoka Barcelona. ***(90min)***

### LAMPARD AITAKA OXFORD

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Everton, Frank Lampard yuko katika kinyang'anyiro cha kuwania nafasi ya ukocha katika klabu ya Oxford United ya League One. ***(Sun)***

### JAYDEN AIVUTIA UNITED

KLABU ya Manchester United inavutiwa na mshambuliaji wa AZ Alkmaar raia wa Uholanzi, Jayden Addi. ***(Football Transfers)***

### ALONSO KUONDOKA BARCA

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Hispania, Marco Alonso, 32, anatarajiwa kuondoka Barcelona na kujiunga na wapinzani wao wa LaLiga, Atletico Madrid. ***(Football Transfers)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ENRIQUE HAFURAHII KAZI ANAYOFANYA MBAPPE

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Mkuu wa Paris Saint-Germain, Luis Enrique, amesema "sina furaha sana" na Kylian Mbappe, licha ya fowadi huyo wa Ufaransa kufunga mabao matatu 'hat trick' na kuifanya timu yake kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, kwa ushindi wa 3-0 dhidi ya Reims, Jumamosi.

**PSG ambao walikuwa ugenini hawakuchukua muda kupata bao la kwanza wakati Ousmane Dembele alikimbia na mpira kwa kasi chini upande wa kulia na kutoa krosi nzuri kuelekea lango la Reims.**

Mbappe aliuwahi mpira kutoka ndani ya eneo la hatari na kupiga shuti la mguu wa kulia lililompita golikipa wa Reims, Yehvann Diouf kwenye kona ya pili baada ya dakika mbili pekee.

Hilo lilikuwa bao la 11 kwa Mbappe kwenye Ligi ya Ufaransa msimu huu, na pasi ya nne ya Dembele. Mbappe baadaye alifikisha mabao 13 msimu huu, akiwa amecheza mechi 11 pekee.

**●●● Sijafurahishwa sana na Kylian, kwa sababu makocha ni wa ajabu, nitamwambia...**

Lakini kocha wa PSG Enrique hakuridhika.

"Sijafurahishwa sana na Kylian leo," alisema Enrique akiiambia Amazon Prime.

"Kwa nini? Kwa sababu makocha ni wa ajabu sana. Kuhusu mabao, sina la kusema, sina malalamiko. Lakini nadhani anaweza kuisaidia timu kwa njia tofauti kwa sababu yeye ni muhimu sana.

"Nitamwambia kwanza, na baada ya hapo sitawaambia kwa sababu haiko hadharani. Tunadhani Kylian ni mmoja wa wachezaji bora duniani, bila shaka kuhusu hilo, lakini tunahitaji zaidi na tunamtaka afanye zaidi, hayo ni maoni yangu."

PSG, ambao walipoteza kwa AC Milan katika Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne, walikuwa na wakati mzuri katika Jiji la Champagne na kutumia nafasi walizozipata.

Mbappe aliifungia timu yake bao la pili dakika ya 59 baada ya pasi ya Dembele, ambaye alimpita kirahisi Carlos Soler na kutengeneza njia rahisi kwa Mbappe.


Reims waliadhibiwa kwa bao la tatu wakati Mbappe alipochezewa madhambi eneo la hatari na Bradley Barcola na akafungwa kwa mkwaju wa penalti dakika ya 82.

Mbappe alikaribia kuongeza bao la nne kwa mkwaju mkali kutoka pembeni mwa kisanduku ambapo shuti lake liligonga mwamba.

Alipoulizwa kuhusu uchezaji wake mwenyewe, Mbappe aliiambia Amazon Prime: "Kwa kiasi kikubwa sihitaji kucheza vizuri ili kufunga mabao, lakini nataka kufanya yote mawili, kufunga mabao na kucheza vizuri. Hilo ndilo lengo langu, kusaidia kila wakati timu kama niwezavyo."

Ushindi wa tano mfululizo wa ligi uliifanya PSG kuwa pointi moja juu ya Nice, huku Reims wakiwa katika nafasi ya nne, pointi saba nyuma ya vinara.

# MIKEL ARTETA AMMWAGIA SIFA KIBAO TROSSARD




**LONDON,** England

MIKEL Arteta alisifu kiwango cha Leandro Trossard wakati Arsenal ilipopata ushindi muhimu dhidi ya Burnley kwenye Ligi Kuu, Jumamosi.

Fowadi huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28, alifunga bao la kwanza dakika za mwisho za kipindi cha kwanza, kabla ya kutoa pasi nzuri kwa William Saliba na kurejesha uongozi kwa 'Washikabunduki' hao baada ya Josh Brownhill kusawazisha.

Oleksandr Zinchenko akafunga la tatu katika dakika ya 74 - huku Fabio Vieira akioneshwa kadi nyekundu kwa mchezo mbaya.

Baada ya mafanikio hayo magumu, kocha Arteta alisifu kiwango cha Trossard kwenye mchezo huo.

Alisema: "Lazima uweke mwili wake juu ya mstari ikiwa ni lazima na yeye Trossard amefanya hivyo.

"Pia ni bao la 1000 kwenye Uwanja wa Emirates, namba nzuri, kwa hiyo nina furaha naye sana.

"Nadhani kila wakati unapomuuliza acheze, iwe kati au kama namba tisa, anakuwa tishio la kweli, kwa hiyo ninamfurahia sana yeye."

Ushindi huo umeifanya Arsenal kuwaruka mahasimu wao Tottenham Hotspur, ambao walipokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Wolves mapema siku hiyo, na kuwa juu yao kwa pointi moja, huku vinara Man City jana Jumapili walitarajiwa kucheza na Chelsea.

Baada ya kufikia mapumziko mengine ya kimataifa, Arteta alisisitiza umuhimu wa kuongeza kasi na kuhakikisha wachezaji wanarudi nyuma kabla ya ratiba yenye shughuli nyingi za msimu wa baridi.

Aliongeza: "Hivi ndivyo timu hii inavyofanya. Tunacheza kwa njia bora zaidi, tunatoa kila kitu kushinda michezo.

"Inatupa kasi. Tunahitaji kuwarejesha wachezaji kwa sababu kwa sasa tuna wachezaji wanane ambao hawajapatikana na ni wengi, na Desemba tuna michezo 11 inayokuja, hivyo bora tuwarudishe kila mtu haraka.

# Ancelotti amtoa Bellingham

**MADRID,** Hispania




CARLO Ancelotti amesema bega la Jude Bellingham litapimwa na timu ya madaktari wa England kabla ya mapumziko ya kimataifa, lakini akasisitiza kiungo huyo "hawezi kuicheza na timu ya taifa" baada ya kukosa kwenye ushindi wa mabao 5-1 wa Real Madrid kwenye LaLiga dhidi ya Valencia, Jumamosi.

Huku Bellingham akitazama kutoka jukwaani, Vinicius Junior na Rodrygo kila mmoja alifunga mabao mawili kwa Madrid baada ya Dani Carvajal kufunga bao la kwanza pale Santiago Bernabeu, huku Hugo Duro akifunga la kufutia machozi kwa Valencia.

Bellingham awali alikuwa ametajwa kwenye kikosi cha Madrid siku ya mechi, lakini akajiondoa mapema Jumamosi, klabu hiyo ikisema "aligundulika kuwa bega la kushoto lina maumivu, matokeo ya kuvunjika kwake hivi karibuni" dhidi ya Rayo Vallecano wikendi iliyopita.

"Atatathminiwa na England," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Kama hakucheza leo (juzi), hawezi kucheza na timu ya taifa. Atafanya kazi maalum kwenye bega lake. Baada ya mapumziko anaweza kucheza tena."

England itacheza na Malta na Macedonia Kaskazini katika mechi ya kufuzu kwa michuano ya Ulaya wiki hii.

Bellingham alikuwa amefunga mabao 13 katika mechi 13 za Madrid kabla ya jeraha lake, na kulikuwa na shinikizo kwa Vinicius na Rodrygo kufanya vizuri bila yeye.

"Wote wawili (Vinicius na Rodrygo) wamerejea katika kiwango chao bora," alisema Ancelotti.

"Walihitaji muda tu kuonesha sifa zao bora. Katika michezo miwili iliyopita wamefanya vema, wakichanganya vizuri kutafuta nafasi na kuonyesha ubora wa ajabu. Tunaweza kusema kwamba wamerejea."

## Majeruhi yaitesa Man Utd

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United wamepata pigo baada ya majeruhi mapya ya Rasmus Højlund na Christian Eriksen baada ya ushindi wao wa 1-0 dhidi ya Luton Town, Jumamosi.

Højlund alitolewa kipindi cha pili na tatizo la misuli ya paja huku Eriksen akilazimika kutolewa nje katika kipindi cha kwanza kutokana na jeraha la goti.

Ni habari mbaya zaidi kwa kocha Erik ten Hag, ambaye tayari hana Casemiro, Lisandro Martinez, Luke Shaw, Tyrell Malacia na Jonny Evans.

Aaron Wan-Bissaka alikosa ushindi dhidi ya Luton kwa sababu ya ugonjwa huku Jadon Sancho akisalia nje ya kikosi cha kwanza kwa sababu ya suala la kinidhamu.

"Kwa wakati huu siwezi kusema chochote kuhusu hilo jeraha la Højlund kwa sababu sijui," alisema Ten Hag mara baada ya mchezo wa Jumamosi.

"Tunafanya tathmini, lakini inabidi tusubiri kwa saa 24 ili kuona hitimisho ni nini. Wape madaktari wa timu saa 24 kuona tatizo ni nini, kama kuna tatizo."

Kuachwa kwa muda mrefu kwa Højlund, ambaye amejiweka kuwa chaguo la kwanza la mshambuliaji wa United baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 72 kutoka Atalanta msimu wa majira ya joto, itakuwa pigo kubwa kabla ya mechi ngumu za ugenini dhidi ya Everton, Galatasaray na Newcastle United baada ya mapumziko ya kimataifa.

"Hatutaki kupoteza mchezaji yeyote na ni sawa kwa Christian Eriksen, lakini huu pia ni msimu wetu, majeruhi wengi," Ten Hag aliongeza.

"Kwa hiyo una kikosi. Lakini tunazungumza mara nyingi, viwango vya kawaida katika timu yako, katika njia ya uchezaji. Tunatumaini wachezaji wanarejea."

Marcus Rashford, ambaye amefunga bao moja pekee katika michuano yote msimu huu, na Alejandro Garnacho wote walipoteza nafasi nzuri.

# HABARI MICHEZO

## Gamondi ataja ilipo jeuri yake

INATOKA UKURASA 24

zitakazoivusha kwenda hatua ya robo fainali.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema mkakati huo utajumuisha viongozi, benchi la ufundi, wanachama na mashabiki wa timu hiyo ambapo kila mmoja atakuwa na jukumu la kuhakikisha timu hiyo inasonga mbele na kufikia hatua ya robo fainali kwa pointi tisa za nyumbani.

"Tupo kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini asikudanganye mtu, ukifika hatua hii ili usonge mbele na kufika robo fainali ni lazima uchukue pointi tisa za nyumbani, na sisi kama Yanga mchezo wetu wa kwanza nyumbani tutacheza na Al Ahly ya Misri Desemba 2, ukiacha wa kwanza wa ugenini Novemba 24 dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria.

"Wanachana na mashabiki wa Yanga tuna kazi moja tu Desemba 2, tutakuwa na mchezo mgumu sana dhidi ya Al Ahly, lakini kutokana na umoja tulionao hakuna mchezo mgumu kwa Yanga, na niseme tu msimu uliopita tulifika fainali kwenye Kombe la Shirikisho la Soka Afrika, msimu huu kuna jambo letu lingine tunalolitafuta," alisema.

Akifafanua hilo, Kamwe alisema wanachama na mashabiki wao watakuwa na kazi moja tu ya kuja uwanjani na kujaza uwanja wa Benjamin Mkapa ili kuwashangaza wageni, ambapo benchi la ufundi kazi yake itakuwa ni kuwasuka, kuwatengeneza na kuwapa mbinu na ujanja wachezaji.

## Kocha Mualgeria, Mtunisia watajwa

INATOKA UKURASA 24

hana shida kwa sababu anafahamu Tanzania ni nyumbani na Simba ni sehemu ya familia yake kwa sababu aliwahi kuifundisha klabu hiyo.

"Rwanda na APR, Simba ni nyumbani na kama hilo jambo litaenda vizuri nitakuwa sehemu ya benchi hilo la ufundi ila ni mapema kusema lolote kwa sasa," alisema Adel ambaye amekuwa akiitakia kheri Simba kila inapokaribia michezo mikuwa na kuwapa pole wanapopata matokeo mabaya ikiwamo mechi iliyopita dhidi ya Yanga.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema uongozi upo katika mchakato huo na wakati wowote kuanzia kesho wanaweza kumtangaza kocha mkuu ambaye atakuja kuchukuwa mikoba ya Robertinho.

# RAGE ATAKA KAMBI SIMBA IPELEKWE Z'BAR KUIUA ASEC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikitajwa kuwa huenda Simba ikamtangaza kocha wa zamani wa USM Alger ya Algeria, Abdelhak Benchikha, kuwa Kocha Mkuu wa kikosi hicho, rais wa zamani wa klabu hiyo, Ismail Aden Rage, amewashauri viongozi kuweka kambi mjini Zanzibar ili kuepuka utoro uliokithiri wa wachezaji wawapo Dar es Salaam jambo litakalowasaidia kupata matokeo dhidi ya Asec Mimosas.

**Simba itaikaribisha Asec Mimosas ya Ivory Coast kwenye mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Novemba 25, mwaka huu.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Rage pia aliwataka viongozi wa Klabu ya Simba kuwa wajasiri, na kuwa na tabia ya kuzungumza na vyombo vya habari pale inapotokea sintofahamu kama iliyopo sasa, badala ya kumuachia Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, pekee.

Rage alisema ana taarifa ambazo bado anaendelea kuzitafutia uthibitisho kuwa wachezaji wa Simba hawakulala kambini siku moja kabla ya mechi ya Yanga, badala yake walirejea asubuhi, ndipo jioni yake ikatandikwa mabao 5-1 Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Moja ya sababu iliyotufanya tufungwe, inasemekana sina uthibitisho, lakini viongozi wanaweza kukanusha kama siyo kweli, lakini ukweli ni huu, baadhi ya wachezaji wakubwa hawakulala kambini, wamekuja asubuhi siku ya mchezo, huo ni utovu wa nidhamu wa hali ya juu, unatakiwa kiongozi uwe jasiri, unamwambia fulani hujalala kambini, tunakusimamisha tutakujadili kwenye kamati ya maadili, lakini jamani bado wanakwenda wanacheza na baya zaidi mashabiki wetu wanafanya makosa, kuna wakati kocha anaona mchezaji fulani hachezi vizuri wanaanza kumtukana, kwa hiyo tatizo lilikuwa ni hilo lazima tukiri kuna udhaifu kwa viongozi wetu," alisema Rage.

Alisema baadhi ya wachezaji wa kigeni wakifika nchini husahau kilichowaleta na kujitumbukiza kwenye mambo yasiyofaa.

"Dar es Salaam kwa wachezaji wetu hawa wa kigeni, hapa ni pepo yao hii, watu ambao hawajui Jiji la Dar, limebadilika sasa hivi, lina maeneo mengi ya starehe, kwa hiyo hawa wageni wanapokuja na wanalipwa pesa nyingi, akichukua dola yake mia moja tu anapata laki mbili na nusu, na bia moja ni Sh 1,500, anakunywa anavyotaka na atafanya upuuzi wake wote wanaotaka, ndiyo maana tunasikia wachezaji mara wametoroka au hawataki kukaa kambini, moja ya sababu ni hii," alisema.

Kwa sababu hiyo alisema wachezaji hawa wanatakiwa kuangaliwa kwa ukaribu na kuwa na viongozi wakali wenye msimamo.

"Natoa ushauri kwa viongozi wangu, wawakusanye wachezaji wawapeleke kambi Zanzibar, mimi wakati wa uongozi wangu niliwapa heshima sana watu wa Zanzibar, kila mechi kubwa nilikuwa nawapelekea timu, kule pia kuna nidhamu, huwezi kukuta mtu katoka kwenda disco, hakuna ujinga wa namna hiyo.

"Kwa hiyo nashauri katika mashindano haya si lazima kwenda nje kuweka kambi wala Dar es Salaam, wawakusanye wachezaji wawapeleke kambini Zanzibar, wakirudi nakuhakikishia Asec Mimosas watalia," alisema Rage ambaye hivi karibuni na wenzake 20 waliteuliwa na Rais wa Heshima wa Simba, Mohamed 'Mo' Dewji kuwa wajumbe wa Baraza la Ushauri la Klabu.

Pia aliwataka viongozi wawe wanajitokeza linapotokea jambo zito kama la kufungwa mabao 5-1 na watani wa jadi na kuwachanganya Wanasimba wote ambao kwa sasa wanahitaji faraja kutoka kwa viongozi wao.

"Kwa jambo kama hili ilifaa viongozi wetu wajitokeze na waongee na wanachama na mashabiki wao, mabao matano ni mengi, bado wamekaa kimya na wamemuachia msemaji tu, kwani watu wa habari huwa wanawatisha viongozi wetu? Maana siyo jambo gumu au baya kuongea na waandishi wa habari wanakusaidia, ingawa wakati mwingine mna maswali ya kuudhi," alisema Rage.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salum Abdallah 'Try Again' akiwa na tuzo ya mashabiki bora wa michuano ya African Football League (AFL), aliyokabidhiwa baada ya mechi ya fainali kati ya Mamelodi Sundonws na Wydad Casablanca ya Morocco ambayo ilipigwa Uwanja wa Loftus Versfeld, Pretoria Afrika Kusini jana. Mamelodi ilitwaa ubingwa kwa kushinda 2-0 huku ushindi wa jumla ukiwa 3-2 baada ya fainali ya kwanza nchini Morocco Novemba 5, mwaka huu, kufungwa 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Dullah Mbabe kujiuliza tena kwa Katompa wiki ijayo

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Abdallah Pazi 'Dullah Mbabe', anatarajia kupanda ulingoni kwa mara ya pili kurudiana na Tshimanga Katompa wa DR Congo katika pambano la raundi kumi linalotarajiwa kupigwa Novemba 25, mwaka huu, kwenye Ukumbi wa AICC jijini Arusha.

Dullah Mbabe atapanda ulingoni katika pambano hilo la raundi kumi akiwa na rekodi za kuchezea kichapo kizito katika pambano la kwanza ambalo lilipoteza utawala wake nchini.

Pambano hilo limeandaliwa na Kampuni ya Red in Lady Promotion chini ya Mbunge wa Viti Maalum, Susan Mwakagenda, huku likipewe jina la 'The Jungle Fight'.

Mbali ya pambano hilo kuu, mabondia wengine watakaopanda ulingoni siku hiyo kulisindikiza ni Paul Kamata atakayezipiga na Jacob Maganga wakati Loren Japheth akitarajiwa kuzichapa na Rilwal Liwan wa Nigeria.

Wenginne ni Shaban Kaoneka akipewa Kassim Somboko wakati Shaban Ndaro akipewa Saleh Mkalekwa huku Chiku Idd akitarajiwa kukiwasha na Leilaj Macho.

Mkongwe wa Kilimanjaro, Alibaba Tarimo, anatarajiwa kumvaa Karage Suba 'Mzee wa Gadi Kibanda' huku Sarah Alex 'Miss GB wa Chuga akitarajiwa kumalizana na Tatiana Ezekiel.

# Michezo

Jumatatu Novemba 13, 2023

Nipashe





## Arteta ammwagia sifa Trossard

UKURASA 22




Wachezaji, viongozi na benchi la Ufundi la Mamelodi Sundonws wakisherehekea kutwaa ubingwa wa African Football League (AFL), baada ya kuichapa Wydad Casablanca ya Morocco mabao 2-0 kwenye fainali ya pili iliyopigwa Uwanja wa Loftus Versfeld uliopo Pretoria Afrika Kusini jana. Memelodi ambayo inakuwa timu ya kwanza kubeba taji hilo lililoanzishwa msimu huu, imetwaa ubingwa huo kwa ushindi wa jumla wa mabao 3-2 baada ya fainali ya kwanza nchini Morocco Novemba 5, mwaka huu, kufungwa 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# GAMONDI ATAJA ILIPO JEURI YAKE YANGA SC

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## Nzengeli, Pacome, Aziz Ki nao wahusishwa, huku uongozi ukianika mkakati Ligi ya Mabingwa...

HUKU uongozi wa Yanga ukianza kuandaa mikakati ya namna ya kuvuna alama zote tisa kwenye mechi zake za nyumbani za hatua ya makundi za Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameanika kinachompa jeuri ya kutoona sababu ya kuwa na mshambuliaji asilia katika kikosi chake.

**Yanga hadi sasa imecheza mechi tisa ikitikisa nyavu mara 26 na kuruhusu mabao matono, Stephen Aziz Ki na Max Nzengeli wakiwa vinara wa kufunga ndani ya timu hiyo kila mmoja akicheka na nyavu mara saba na manne yakifungwa na Pacome Zouzoua.**

Washambuliaji Hafiz Konkoni na Clement Mzize kila mmoja amefunga mabao mawili huku kiungo mkabaji Mudathir Yahya na beki wa kati, Dickson Job kila mmoja akifunga moja.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha huyo alisema mipango yake katika kufundisha anawapa uhuru wachezaji wake hasa mwenye uwezo wa kutumia nafasi anaweza kufunga na si lazima mshambuliaji.

Alisema wachezaji wote wana kazi ya kupambania timu uwanjani ili kutafuta ushindi, na lazima kila mmoja kuwa makini kutumia vizuri nafasi zinazopatikana bila kujali anacheza nafasi gani.

"Mipango yangu kila mchezaji anatakiwa kutumia nafasi zinazopatikana akiwa sehemu nzuri kufunga, anatakiwa kufanya jukumu hilo, kila mtu yupo huru kupambania timu kupata matokeo chanya.

Ukiangalia mabao tuliyofunga mengi yamefungwa na viungo, washambuliaji hawajafunga mabao mengi, hii ni jinsi gani ninavyotaka kwa wachezaji wangu hasa katika kushirikiana kutimiza majukumu," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa viungo wanafunga mabao mengi na mabeki watafanya hivyo kwa kuwa anawapa uhuru wa kufunga ili kuipa timu matokeo mazuri na kufikia malengo yao.

Gamondi alisisitiza kuwa anahitaji kuona matokeo mazuri katika kila mechi jambo ambalo wachezaji wake wanatambua na kila mmoja kuhakikisha anatimiza majukumu anayopewa siku ya mechi.

Kuhusu maandalizi ya mchezo ujao wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad, Algeria, alisema mazoezi yanaendelea kwa wachezaji ambao hawako kwenye majukumu ya timu za taifa.

"Tumefanikiwa kuwaangalia wapinzani wetu baadhi ya mechi zao na kuona ubora wao kikubwa ni maandalizi yetu kuelekea mchezo huo ni muhimu kupata matokeo mazuri ugenini," alisema Gamondi.




Katika hatua nyingine uongozi wa klabu hiyo, umesema kwa sasa inandaa mikakati ya kuhakikisha inashinda mechi zake zote tatu za Ligi ya Mabingwa Afrika itakazocheza nyumbani, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ikiamini ndizo

INAENDELEA UKURASA 23

# Kocha Mualgeria, Mtunisia watajwa kutua Simba SC

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba uko kwenye mazungumzo na makocha wawili, aliyekuwa Kocha Mkuu wa USM Alger ya Algeria, Abdelhak Benchikha na wa Viungo wa APR ya Rwanda, Adel Zrane raia wa Tunisia ili kuja kukinoa kikosi cha timu hiyo.

Benchikha ambaye ni raia wa Algeria, anatajwa kuja kuchukuwa nafasi ya Robertinho Oliveira huku Zrane ambaye aliwahi kuwa sehemu ya benchi la ufundi la Simba akitarajiwa kurejea ndani ya klabu hiyo kuchukuwa nafasi ya Corneille Hategekimana.

Taarifa za uhakika zilizofikia Nipashe kutokana chanzo chetu ndani ya uongozi wa klabu hiyo, zimeeleza kuwa wapo katika mazungumzo hayo na mapema ndani ya wiki hii watakamilisha na hususan kocha wa viungo kabla ya kumalizika kwa mapumzuko ya Kalenda ya Fifa.

Mtoa habari huyo alisema katika meza ya Bodi ya Wakurugenzi Simba, imepokea majina ya makocha wengi akiwamo Sven Vandenbroeck na Benchikha, ambaye jina lake limepita na kuanza mchakato wa mazungumzo naye mapema.

"Tunahitaji kufanya haraka mchakato wa kupata kocha mkuu na wa viungo, hao (Benchikha na Zrane) wamekuwa katika chaguo na mazungumzo yakienda vizuri kwa pande zote mbili wakikubaliana watakuwa sehemu yetu ya benchi la ufundi.

Tunahitaji kufanya mchakato huo mapema ili timu inapokwenda katika mashindano ya kimataifa, mchezo wetu wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas tuwe tumeshampata kocha mkuu," alisema mtoa habari huyo.

Alipotafutwa Adel, alisema

INAENDELEA UKURASA 23



9 770856 541002 >